**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Arobaini na Nne – Tarehe 16 Agosti, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hazi zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA HAIDI MKULO):**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za *Consolidated Holding Corporation* kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2005 *(The Annual Report and Audited Accounts of the Consolidated Holding Corporation for the year ended 31st December, 2005)*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 413

**Nyumba kwa Wafanyakazi**

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA (k.n.y. MHE. SAVELINA S. MWIJAGE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia nyumba za kuishi wafanyakazi wapya wanaoajiriwa au kuhamishwa na kupangiwa vituo vya kazi nje ya Mikoa yao?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida, Serikali ina wajibu wa kuwatafutia nyumba wafanyakazi na viongozi wenye stahili ya kupewa nyumba na Serikali kwa mujibu wa

masharti ya ajira zao. Kwa hiyo, wafanyakazi wa aina hii, wawe wapya au wanaohamishwa na kupangiwa vituo vipya vya kazi, hupewa nyumba au posho ya nyumba pale ambapo nyumba ya Serikali haijapatikana. Serikali haina jukumu la kimkataba kuwatafutia nyumba watumishi wengine wasio na stahili.

Hata hivyo, kutokana na uamuzi wa Serikali wa kuuzia watumishi na viongozi wa Serikali nyumba za zamani walizokuwa wanaishi, watumishi na viongozi wa aina hii na ambao wana stahili, wanapohamishwa wakati wamekwishauziwa nyumba katika vituo vyao vya zamani, wanategemewa kupanga nyumba kibiashara au katika nyumba za wakala zilizotengwa kupangishwa kibiashara.

Aidha, Serikali itaendelea kujenga nyumba mpya (*tied quarters)* Mikoani kote kwa ajili ya viongozi na wafanyakazi wenye stahili ya kupewa nyumba na Serikali kwa mujibu wa masharti ya ajira zao. Hizi *tied quarters* hazitauzwa kuanzia sasa. *(Makofi)*

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu uliotumika hivi karibuni kwa Serikali kuuza nyumba zake zote na hasa maeneo kama Dar es Salaam *Oysterbay* na kwingine, zile nyumba ziliuzwa kwa bei iliyo chini ya soko na kwa kuwa inagundulika sasa mahitaji ya nyumba za wafanyakazi wa Serikali ni mengi na yataendelea kuwa mengi: Je, Serikali itakiri kwamba hilo lilikuwa kosa na kwamba haitakaa irudie kufanya hilo kosa tena? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kuanzia sasa nyumba ambazo zitakuwa ziko *tied quarters* hazitauzwa tena. Lakini Serikali inafanya jitihada zote kuhakikisha kwamba wale watumishi na viongozi ambao wanastahili ya kupewa nyumba kwa mujibu wa ajira zao, wanapata nyumba na ndiyo maana nimeeleza katika jibu la msingi kwamba, Serikali inaendelea kujenga nyumba kila mahali Mikoani na Wilayani ili wale watumishi wanaostahili wapewe nyumba.

Mheshimiwa Spika, sio kweli kwamba Serikali ilifanya makosa kuuza nyumba zile ambazo zilikuwa ni za zamani na matengenezo yalikuwa yanaigharimu sana Serikali. Serikali kwa sasa hivi baada ya uamuzi huo inaendelea kujenga nyumba na ndio maana unakuta kwamba, nyumba za sasa, viongozi ambao wamepewa nyumba na hata Mawaziri wa sasa wanakaa katika nyumba mpya kabisa na safi. *(Makofi)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wabunge, wanaoishi Kisasa ni sawasawa na viongozi wengine na kwa kuwa katika zile nyumba zilizoko kule, baada ya Wabunge kuhamia kule walinzi wote wamehamishwa na zile nyumba hazina usalama kabisa sasa hivi na hata *fence* bado haijajengwa: Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kuwezesha hata Wabunge wale wapate usalama unaostahili? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, baada ya zile nyumba za Kisasa kukamilika na kukabidhiwa, ilikuwa ni budi wale *JKT* au Wajenzi na Magereza waondoe walinzi wao.

Kwa sasa utaratibu unafanyika kati ya *TBA* na Ofisi ya Spika kuangalia kwamba tunapata kampuni ya ulinzi inayoweza kulinda eneo lile ili mali za Wabunge na usalama wao uwe safi. Lakini vile vile katika Bajeti ya mwaka huu, suala la kuweka *fence* eneo la Kisasa limezingatiwa na litashughulikiwa. *(Makofi)*

Na. 414

**Ujenzi wa Madaraja ya Mito iliyopo Kisesa**

**MHE. LUHAGA J. MPINA** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na tatizo la usafiri kwa wananchi wa Kisesa kutokana na kukosekana kwa madaraja katika Mito ya Igobe, Tindabuligi na Sekasaka:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga madaraja katika mito hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mbunge wa Kisesa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, madaraja yaliyotajwa kwenye swali la Mheshimiwa Mbunge, yapo kwenye barabara ya Mkoa ya Mwandoya - Sakasaka. Madaraja yanayotumika kwenye mito iliyopo Kisesa ni ya aina ya *drift* na huruhusu maji yapite juu na yanapokuwa mengi zaidi, magari na wapita njia hawana budi kusubiri yapungue na hii ndiyo sababu inayoleta kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itajitahidi kubadilisha madaraja haya kwa awamu kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kwenye barabara ya Mwandoya – Sakasaka. Kwa mfano, Serikali imetenga fedha katika mwaka huu wa fedha 2006/2007 ili kujenga daraja kwenye Mto Igobe. Ujenzi wa madaraja mengine kwenye Mito ya Tindabuligi na Sakasaka utaendelea kufanyika kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini ninalo swali moja. Kwanza niipongeze Serikali kwa kukubali kujenga Daraja la Mto Igobe, Daraja la Mto Simiu liliko Jimbo la Kisesa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mito iliyobaki Sakasaka na Tindabuligi ni muhimu sana kwa shughuli za uchumi na kwamba wananchi wengi wamepoteza maisha kwa kuchukuliwa na mito hiyo kwa kuuwawa na mamba na viboko walioko katika mito hiyo: Je, Naibu Waziri, atalidhibitishia Bunge lako kwamba katika madaraja yale yaliyobaki mawili, yaani Tindabuligi na Sakasaka yatajengwa katika Bajeti ijayo ili kunusuru maisha ya wana Kisesa na uchumi wao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoahidi katika jibu langu la msingi, madaraja hayo matatu yatajengwa na kwa kuanzia mwaka huu tunajenga Daraja la Mto Igobe. Kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameomba katika mwaka ujao wa fedha, basi daraja la Tindabuligi na Sakasaka na yenyewe yatajengwa. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa matatizo wanayoyapata wananchi wa Jimbo la Kisesa, hasa katika mito ya Igobe, Tindabuligi pamoja Sakasaka yanafanana sana na matatizo wanayoyapata wananchi wa Mikoa ya Rukwa, Tanga na Mwanza ambao wako katika miradi ya *PMMR* ambayo Serikali mwanzoni kabisa mwa Mkutano huu wa Bajeti, iliahidi na ikatuambia kwamba ujenzi wa mradi huo uko mbioni:

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, anaweza kutuambia sasa hatua zilizofikiwa katika kuanza kutekeleza mradi huo ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, mradi alioutaja wa *PMMR* uko katika maandalizi ya kutekelezwa katika Mikoa hiyo mitatu ambapo mradi huo unatekelezwa na mimi ningemshauri Mheshimiwa Mbunge na wananchi husika wawe na subira wakati *procurement process* ya mradi huu kwanza zikamilike ili mradi huo kuanza kutekelezwa. Najua kwamba mradi umechelewa lakini nadhani ni afadhali usubiri lakini tupate yale ambayo tunategemea kwa maana ya miradi hiyo kuanza kutekelezwa. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri, nilitaka kuuliza kuhusu suala lenyewe la madaraja. Yapo madaraja ambayo yalikuwa yameng’olewa na mafuriko katika barabara inayotoka Mtwara mpaka Masasi hasa katika Mito ya Nangoo, Chikukwe, Makongwa na kadhalika ambayo Wizara yake inayafahamu kabisa. Je, kuna mpango gani wa kurudisha miundombinu katika hali yake ya zamani ikitiliwa maanani kwamba madaraja haya yaling’olewa toka mwaka 1990? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba haya madaraja yaliondolewa na sababu kubwa ilikuwa ni kwamba yalifikia muda ambao kwa kweli yasingeweza kuendelea kuhudumia wananchi. Tatizo ambalo limekuwepo katika kurudishia madaraja ambayo yanakidhi haja ni ukosefu wa fedha. Lakini kwa kadri fedha zinavyozidi kupatikana tuta-*replace* madaraja hayo aliyoyataja kulingana na upatikanaji wa fedha katika Wizara yetu. *(Makofi)*

Na. 415

**Utaratibu wa Kukiimarisha Kitengo cha Hali ya Hewa**

**MHE. RICHARD M. NDASSA** aliuliza:-

Kwa kuwa dunia ya sasa inabadilika, kila kukicha na mazingira yake yanaharibiwa kwa namna mbalimbali na kuna majanga mengi ambapo asilimia kubwa husababishwa na hali ya hewa na kwa kuwa ukijua hali hali ya hewa ya siku zijazo husaidia kujihami na kwa kuwa upatikanaji wa taarifa zenye uhakika kuhusu hali halisi ya hewa badala ya utabiri wa hali ya hewa unaofanywa sasa hivi unahitaji kuwa na watalaam na ujuzi wa kutosha pamoja na kuwa na vifaa na vyombo vya kisasa vya kuweza kung'amua hali halisi ya hali ya hewa:-

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kukiimarisha Kitengo cha Hali ya Hewa kwa kukipatia vifaa vya kisasa, ikiwa ni pamoja na kuwapa wafanyakazi mafunzo ya kutosha, hivyo kusaidia upatikanaji wa taarifa halisi ya hali ya hewa badala ya kupewa taarifa ya utabiri wa hali ya hewa?

**SPIKA:** Kwa faida ya wageni, nilikuwa napenda kuwafahamisha kwamba hii ni mojawapo ya Wizara ambazo zina Naibu Mawaziri wawili. Kwa hiyo, wa kwanza niliyemuita Naibu Waziri ni Mheshimiwa Dr. Milton M. Mahanga na huyu sasa ni Dr. Maua Daftari.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli utabiri sahihi wa mwenendo wa hali ya hewa hutegemea vifaa vya kisasa na utaalam wa kutosha wa shughuli za utabiri. Serikali imechukua hatua mbalimbali za makusudi za kuimarisha mamlaka ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2000 hadi sasa mamlaka imetafuta misaada toka nchi mbalimbali wahisani na imefanikiwa kupata vifaa vifuatavyo:-

Katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2003/2004 hadi mwaka 2005/2006 Mamlaka ya Hali ya Hewa imepokea misaada mbalimbali toka nchi wahisani na mashirika mbalimbali ya wahisani kama ifutavyo:-

(a) Benki ya *BADEA* imetoa msaada wa vifaa mbalimbali vyenye thamani ya *USD* 368,658;

(b) Shirika la Hali ya Hewa Duniani limetoa vifaa vya aina mbalimbali vyenye thamani ya *USD* 360,000;

(c) Pia tulipokea msaada na vifaa vya kukabiliana na majanga kutoka Ufaransa vyenye thamani ya *USD* 840,000; na

(d) Umoja wa Ulaya na Shirika la *ALCATEL* walitoa msaada wa uimarishaji mitambo ya mawasiliano wenye thamani ya *Euro* 53,739 na *USD* 100,000.

Mheshimiwa Spika, mamlaka imejitahidi kuendelea kunyanyua kiwango cha taaluma kwa wafanyakazi wake wa kada mbalimbali, ndani na nje ya nchi kuanzia mwaka 2000 hadi sasa. Mafunzo hayo mengi yamegharamiwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa, yenyewe na mengine kwa kushirikiana na nchi wahisani kama vile Urusi, *WMO*, India, *UK*, China na kadhalika na yamehusu taaluma za masuala ya hali ya hewa, uhandisi, uhasibu, uongozi, ngazi za shahada, stashahada na udaktari wa falsafa na hata pia udereva na mafunzo ya Sekondari.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi, tunao watalaamu na mabingwa wa utabiri wa hali ya hewa 122 na wasaidizi 210. Lengo la mamlaka katika kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wake ni kuhakikisha kuwa wanakuwa na watalaam wa kutosha na wenye uwezo watakaoziba pengo mara baada ya wengine kufikisha umri wa kustaafu. Wafanyakazi hao wamekuwa chachu ya mafanikio kutokana na juhudi mbalimbali wanazozionyesha katika kuendeleza sekta hii.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi nimpongeze Mheshimiwa Ndassa kwa kuwa karibu sana na mamlaka hii kwa kutoa mawazo mbalimbali ya kuboresha mamlaka hii. Naamini fika kwamba wapiga kura wake wanafaidika fika na taarifa za hali ya hewa.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika majibu yake ya msingi ameeleza kwamba mamlaka inafanya juhudi kubwa katika kuwaelimisha watumishi wake, lakini pia kwa sababu tunajua umuhimu wa hali ya hewa katika maendeleo ya nchi hii hasa katika uchumi, lakini pia walengwa hasa wengi ambao ni wa Vijijini kwa maana ya wakulima na wafugaji hawaipati elimu hii sawasawa sambamba na kutoa elimu zaidi kwa wafanyakazi: Je, mamlaka hii ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba elimu hii inawafikia wananchi wengi zaidi hasa wakulima na wafugaji wa nchi hii ambao sasa yanawahusu sana masuala ya hali ya hewa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nimpongeze Mheshimiwa Zambi kwa muda wote tuliokuwa naye katika Mamlaka ya Hali ya Hewa, amefanyakazi nzuri ya kusaidiana na wenzake katika kuboresha hali ya hewa.

Pili, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge, kwamba tunayo mikakati mbalimbali ya kuelimisha jamii. Kwanza, tunatoa majarid maalum kila baada ya miezi mitatu ambayo yanasambazwa takwimu za hali ya hewa kwa watu wote.

Pili, tuna *bulletin* inatoka kila baada ya siku kumi kwa ajili ya kutoa taarifa mbalimbali za hali ya hewa. Vile vile, tuna vipindi vya redio ambavyo tunatoa kila wiki. Lakini katika mwaka huu tunategemea kwamba watalaam wa hali ya hewa watafika Vijijini.

Napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge, kwamba utabiri wa hali ya hewa una nafasi nzuri sana ya kusaidia uchumi wa nchi hii na taarifa za hali ya hewa zinasaidia sana kwa wale wanaojenga na kwa wale wanaolima (wakulima) pamoja na ufugaji na tutahakikisha kwamba wafugaji na wakulima wanapata taarifa za hali ya hewa mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mamlaka ya Hali ya Hewa inacho Chuo pale Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji na kwa kuwa vifaa vya kutendea kazi ni pamoja na nyenzo za usafiri, lakini nyenzo alizonazo pale ni chache na zilizopo zimechakaa kwa maana ya magari. Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba ni wakati muafaka sasa wa kukisaidia Chuo kile usafiri ili waweze kufanya kazi za utabiri wa hali ya hewa kwa uhakika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, pale Kigoma tuna Chuo cha Hali ya Hewa na mimi mara kadhaa nimepata nafasi ya kukitembelea Chuo kile. Napenda nimhakikishie kwamba tunajitahidi sana kukiboresha Chuo kile kwa kukipatia vifaa vizuri vya kuendeshea shughuli zake vikiwemo pamoja na vitabu kwa ajili ya kusomeshea wanafunzi wa hali ya hewa. Suala la usafiri tutalishughulikia ipasavyo. *(Makofi)*

## KAULI ZA MAWAZIRI

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tarehe 25 Julai, 2006 wakati wa mjadala wa hoja ya Bajeti ya Wizara yangu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mbunge Viti Maalum, alipata nafasi ya kuchangia hoja hii. Katika mchango wake pamoja mambo mengine alitoa shutuma nzito kwamba kuna wanawake wanaofungwa Magerezani wakiwa hawana ujauzito, lakini baadaye hupata mimba wakiwa Magerezani. Hapa nanukuu kile alichokisema na kunakiliwa na *Hansard* ya siku hiyo.

Naanza kunukuu: “Siku za nyuma kabla sijawa Mbunge, nilikuwa nikiona wafungwa wana mimba, nilikuwa najiuliza: Je, hizi mimba wakati wako jela wanazipata vipi? Nikaja kufuatilia, kuna mwanamke aliyekuwa amefungwa kwa muda wa miaka miwili, anasubiri kumaliza kifungo chake. Baada ya miaka miwili na nusu alionekana ana mimba wakati akifungwa alikuwa hana mimba. Wakati huo huo wanawake wanapokuwa jela huwa wanalindwa na Bibi jela na wanakaa sehemu ambayo iko mbali kabisa na vyumba vya wanaume ambao na wenyewe wamefungwa jela. Sasa cha ajabu ni kwamba, mwanamke huyo anafikisha mwaka mmoja au miwili unakuta ana mimba na wakati huo huo huwa hawana mawasiliano na mume wake. Wakati mume wake anakuja kumwona jela, huwa yule Askari mwanamke anayewalinda naye yuko hapo hapo na wanapozungumza anasikia. Huwa hawaendi faragha. Sasa nashangaa hiyo mimba amepata imetoka wapi mle jela? Naomba kuuliza, huyo mtoto atakayezaliwa baba yake anaitwa nani? Anaitwa jela au Magereza?” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, hoja hii ilitustua sana viongozi wa Wizara hii na pia wananchi waliokuwa wanafuatilia mjadala wa Bunge. Kwani hoja iliashiria kwamba katika Magereza yetu wafungwa wanawake hufanya vitendo vya ngono ama na wafungwa wanaume au na Askari wanaume wa Jeshi la Magereza, jambo ambalo ni uvunjaji wa sheria na maadili ya jamii yetu kwa kiwango kikubwa kabisa.

Kutokana na hoja ya uzito wa hoja hii, Wizara yangu imefanya uchunguzi wa kina katika Magereza yote nchini ili kubaini kuwepo kwa hali hii, kama hoja ya Mheshimiwa Mbunge, ilivyoashiria. Katika uchunguzi huo, tumeangalia taratibu za uendeshaji wa Magereza hasa makazi na shughuli za wanawake wafungwa.

Mheshiiwa Spika, tumekagua kumbukumbu za Magereza yote nchini, tumehoji Kamishna Mkuu wa Magereza Bwana Banzi na tumewahoji Makamishna Wakuu wa Magereza Wastaafu akiwemo Kamishna Mstaafu Mwanguku na Kamishina Mstaafu Malisa, tumewahoji baadhi ya wanawake wafungwa na kadhalika. Matokeo ya uchunguzi wetu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, sheria na taratibu za uendeshaji Magereza nchini, zinahitaji wafungwa wakae kwa kutenganishwa kiumri, jinsi, afya, hali ya uhalifu na kadhalika. Utenganisho huu ni moja ya misingi mikuu ya uendeshaji Magereza hapa nchini. Kwa mujibu wa utenganisho wa kijinsia katika Magereza yetu yote wafungwa wanawake wanawekwa katika eneo lao pekee na tumeona hakuna uwezekano wowote wa wafungwa wanaume na wa kike kuingiliana mahali popote na wakati wowote.

Hali kadhalika, Askari na Maafisa wa Magereza wanaume hawana nafasi yoyote ya kuingiliana na wafungwa na wanawake kwa wazi au kwa faragha. Hata Mkuu wa Gereza, wakati wa ukaguzi wa sehemu ya Gereza wanakoishi wafungwa wanawake ni lazima afuatane na Askari na Maafisa wa kike wakati wote akiwa katika eneo hilo.

Pili, utaratibu uliopo katika Magereza yetu nchini ni kwamba mfungwa mwanamke, anapopokelewa Gerezani kwa mara ya kwanza hupimwa afya yake ikiwa ni pamoja na hali ya ujauzito. Baadhi hupokelewa Magerezani wakiwa wajawazito. Hawa hupatiwa huduma stahiki hadi wanapojifungua na huendelea kuhudumiwa pamoja na watoto wao wakati wote mpaka muda wa kutoka jela utakapotimia.

Tatu, kumbukumbu tulizozipata katika Jeshi la Magereza na baada ya kuwahoji watu mbalimbali zinaonyesha kwamba tangu tupate uhuru mwaka 1961 hadi sasa, hakuna mfungwa wa kike hata mmoja aliyeingia Gerezani hana ujauzito kisha kapata mimba akiwa Gerezani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala hili ni zito na linachafua sura ya Magereza yetu kitaifa na kimataifa, bado mlango uko wazi kwa mwananchi mwenye ushahidi wa hakika atuletee ili Wizara ichukue hatua stahiki.

Katika uchunguzi, tumezungumza pia na Mheshimiwa Mbunge, aliyetoa hoja hii yaani Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, lakini naye hakutusaidia sana, kwani alitueleza kuwa anakumbuka kwamba mwaka 1995 yaani miaka 11 iliyopita alipokuwa

mwanafunzi Muuguzi katika Chuo cha Bombo kule Tanga alipata kusikia tukio hili kutokea katika Gereza la Tanga. Tume-*check* rekodi ya miaka ya nyuma za Magereza yote ya Mkoa wa Tanga lakini hatukupata ukweli wa tukio hili kutokea.

Mheshimiwa Spika, juzi tarehe 13 mwezi wa Agosti nilitembelea Gereza la Isanga nikifuatana na Mheshimiwa Beatrice Shullukindo Mbunge wa Kilindi. Tulipofika sehemu ya wafungwa wanawake katika mambo waliyotulalamikia ni habari waliyoiona na kuisikia kupitia luninga yao hapo Gerezani kwamba wao wanafanya ngono na kupata mimba wakiwa Gerezani. Walitueleza kwamba jambo hili halipo, ni uzushi na pamoja na kuwasononesha, lakini pia limewadhalilisha mbele za waume zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hoja hii imewadhalilisha wanawake wafungwa Magerezani, imewaumiza kisaikolojia Askari na Maafisa wa Jeshi la Magereza na imetoa picha mbaya kwa Jeshi la Magereza, tunamwomba mtoa hoja ama mtu mwingine yeyote mwenye taarifa sahihi atuletee ushahidi wa dhati ili Askari wahusika tuwachukulie hatua za kisheria, kwani kwa Askari wa Gereza kufanya ngono na mfungwa ni kosa la kubaka na adhabu yake ni kufukuzwa kazi na kifungo cha miaka 30 jela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, iwapo mtoa hoja kwa kweli hana ushahidi kamili basi atafanya kitendo cha uungwana kufuta kauli yake na hivyo kuondoa mtafaruku ulioletwa na hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Taarifa hii nilipata kwa mama mmoja ambaye alikutwa na shida hiyo. Lakini sasa hivi sijui mahali alipo. Kwa hiyo mimi nafuta kauli yangu na kuomba radhi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sijapata kwa kuonyesha uungwana. Sio watu wengi wako tayari kukosolewa na kukubali kwamba walikosea au walipotoshwa. Ahsante sana.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu!!

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 41 ya Kanuni za Bunge. Hivi karibuni Mheshimiwa Rais alitoa tamko ambalo lililaani filamu inayohusu minofu ya samaki na sisi Wabunge tuliomba filamu hiyo tuione na tulipoiona filamu hiyo inayohusu suala hilo tuliridhika kuwa filamu hiyo haikuwa na ukweli wowote zaidi ya kutaka kuharibu jina la nchi yetu ikiwa ni pamoja na kuharibu soko la samaki. Kutokana na ukweli huo, Bunge liliamua kulijadili suala hilo na kulitolea uamuzi kupitia Azmio la Bunge.

Mheshimiwa Spika, gazeti liitwalo Uwazi la tarehe 15 Agosti, 2006 ambalo wameandika linaishia mpaka tarehe 21 mwaka huu 2006 limechora picha inayoonyesha

picha inayoonekana ni ya Mzungu na mbwa. Kwa kuiangalia picha hiyo mchoraji aliichora picha hiyo ya Mzungu inayofanana na hali ya kibinaadamu na mtu aliyeonekana kama ni mtu tajiri au bwana mkubwa sana. Lakini kwenye picha hiyo upande wa pili ilichorwa Waheshimiwa Wabunge ambao ndiyo waliolijadili suala hilo kupitia azimio la Bunge kama mbwa wanaobweka.

Kwa kuwa picha hiyo kwa maoni yangu ni kwamba inaua kabisa uamuzi wa Bunge kupitia azimio hilo na kuonekana kwamba Bunge ni kama Taasisi ambayo haina uwezo wowote, kutokana na Kanuni niliyoitaja hapo awali, ni maoni yangu kuwa jambo hili linahusu Haki za Bunge zilizotajwa kwenye Sheria ya Kinga na Madaraka na Haki za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naleta suala hili kwako kwa uamuzi. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ni lazima nikiri kwamba picha hiyo na gazeti hilo nimeonyeshwa asubuhi hii. Linachefua kabisa. Huwezi ukalitazama hilo na ukatoa tafsiri ya kawaida tu ya kusema ni uhuru wa chombo cha habari kuweza kuwaelimisha wananchi juu ya yanayotokea. *(Makofi)*

Kwa hiyo, baada ya kutafakari, nimeamua kwamba Gazeti la Uwazi liombe radhi kwa Bunge ndani ya siku saba na lisipofanya hivyo, basi tutachukua hatua zilizomo katika Sheria ya Madaraka ya Bunge. *(Makofi)*

Azimio lile lilituunganisha vizuri sana na wananchi. Kuweka katika gazeti mchoro unaoonyesha Waheshimiwa Wabunge na Bunge Zima kwamba ni mbwa tena waliokondeana, wasio na uwezo, ni matusi makubwa kabisa kwa Bunge hili.

Kwa hiyo, kama nilivyosema, uamuzi wangu ni kwamba Wahariri, Wachapishaji wa Gazeti la Uwazi waombe radhi ndani ya siku saba, vinginevyo Bunge litachukua hatua za Kikatiba zilizomo katika Sheria zetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mwongozo wa Spika. Mheshimiwa Spika, jambo ambalo limeletwa Mezani na Mheshimiwa Shah hivi punde ni suala zito, nyeti na lenye kuchafua Serikali na Wabunge wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kulitazama tu ghafla ghafla, nahisi bado kwa sababu tunawapa njia wenye magazeti na wengineo hata watu binafsi watafanya makusudi, watukane Viongozi wetu, watukane Mawaziri wetu, anyanyaswe Waziri Mkuu, unyanyaswe wewe mwenyewe kwenye Kiti kitukufu kama hicho. Kwa sababu wanaelewa kwamba Bunge litamwambia aombe radhi.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba Bunge hili letu hili lifikirie njia sahihi ambayo itakuwa muafaka na itakuwa vile vile ni kama pigo kwa wengine wasije wakafanya tena. Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hatua niliyoiamua ni hatua ya awali ya kuona nia ya hawa wenye gazeti. Lakini hatufungwi kuliangalia, maana limekuja sasa hivi na sio wengi mmepata nafasi ya kuliona gazeti na kuweza kutoa maoni yenu. Kwa hiyo, pamoja na kuomba radhi, Bunge lina haki ya kuendelea kulitazama vizuri zaidi.

Naagiza Ofisi ya Katibu wa Bunge aweze kuliangalia vizuri zaidi pamoja na ushauri wa kisheria tuone hatua nyingine za ziada zinazoweza kuchukuliwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

## AZIMIO

### Azimio la Kumwezesha Waziri wa Fedha Kufuta au Kusamehe Maduhuli au Hesabu itokanayo na Upotevu wa Fedha

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulivyomaliza jana, nilikuwa na wachangiaji wawili, Mheshimiwa Godfrey Zambi na Mheshimiwa William Shellukindo na nitawaita kwa mpangilio huo huo.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ili niweze kuchangia kwa kifupi sana hoja ambayo imeletwa na Waziri wa Fedha juu ya taarifa ya upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ukipitia taarifa hii, kwa kweli inasikitisha sana. Suala hili kama lingeletwa mapema lingepata pengine wachangiaji wengi ambao wangehitaji kwa kweli kudadisi mambo ambayo yako ndani ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kuna upotevu wa fedha nyingi sana za Serikali na mimi najiuliza kwamba hivi taratibu za fedha au vifaa au za manunuzi Serikalini zinazingatiwa na kufuatwa kama inavyoandikwa kwenye vitabu vya Sheria?

Mimi naomba kupitia taarifa hii, nitoe mifano michache. Kwenye kitabu hiki ukienda ukurasa wa pili kuna upotevu wa Sh.15,841,000/=. Upotevu huu ulifanywa kati ya Julai, 1994 mpaka Februari, 19 96. Ukiangalia takriban kipindi cha mwaka mmoja na nusu kilikuwa kimepita ndipo kosa likaja kubainika. Lakini kipindi chote hicho kesi imekuja kwenda Mahakamani mwaka 2002, kuanzia mwaka 1996 ilipogunduliwa. Lakini kesi inapelekwa Mahakamani mwaka 2002.

Mimi nikawa najiuliza, kipindi chote hicho cha miaka minne kulikuwa na hatua gani ambazo zilikuwa zimechukuliwa? Lakini pia nikawa najiuliza kwamba, hivi hakuna utaratibu wa Wakaguzi wa ndani kupitia *vouchers* za pesa kila wakati na kabla ya malipo hayajafanywa? Au hatuna hii *Internal Auditing System?*

Mheshimiwa Spika, kama hatuna, basi tuelezwe kwa sababu kulikuwa na muda wa kutosha kumchukulia mhusika hatua, lakini akapewa nafasi mpaka alipoweza kutoroka. Sasa deni lote na hasara hiyo ya milioni 15 linabaki kuwa mzigo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kupitia kitabu hiki, nimeona pia nitoe mfano mwingine wa pili, huu uko kwenye ukurasa wa 14 wa kitabu hiki. Hapo tunaona kuwa kulikuwa na upotevu wa Shilingi karibu milioni 14. Taarifa iliyopo hapa ni kwamba kuna madawa yaliyokuwa kwa ajili ya kutibu maji. Madawa hayo tunaambiwa kwamba yaliharibika. Hapa nikawa najiuliza, madawa haya yaliharibika kwa sababu hayakuwa na mahali pa kutumika au kwa sababu yaliwekwa vibaya? Naamini kwamba madawa haya yanahitajika mahali pengi sana. Mahali pengi sana na ukiangalia inawezekana wakati huo hakukua na madawa ya kutumika kwa ajili ya kutibu maji haya.

Sasa imekuwaje madawa yanatunzwa mpaka yanaharibika na hayajaweza kutumika? Watu walikuwa hawaingii kwenye *store* kuangalia kama mali hizo ziko salama au namna gani? Mimi nadhani kuna *weakness* katika utaratibu mzima wa utunzaji wa mali za Serikali au hata fedha zenyewe za Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna taarifa nyingine ya kusikitisha ambapo ilikuwa chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kuna pesa za *HESAWA* takriban Shilingi milioni 700 zilipotea. Sasa wahusika walipelekwa Mahakamani, lakini cha kusitikisha zaidi tunaambiwa kwamba waliachiwa kwa sababu tu ushahidi haukupatikana wa kutosha. Sasa hili nadhani linasikitisha.

Lakini kinachosikitisha zaidi, unapopita muda mrefu zaidi tangu kosa linapotokea mpaka linapokuja kubainika. Mimi nilikuwa nafikiri pengine ni vizuri sasa Serikali ingejifunza kwamba muda ambao ukaguzi unafanywa kwenye vitabu vya Serikali ni mrefu mno na unawapa *loop hole* wahusika kuweza kuiba wanavyotaka na wenyewe wakaamua mpaka kufanya maamuzi ya kutoroka kabla hawajachukuliwa hatua. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi ningependa kuishauri Serikali kwamba, ichukue hatua inavyostahili mapema inavyowezekana, lakini zaidi tuimarishe *Internal Auditing System.* Tukiimarisha huu ukaguzi wa mara kwa mara mimi nadhani tutaepuka kwa sehemu kubwa makosa ya namna hii au kulitia Taifa letu hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa pia ninaomba sana sana sana wakaguzi wetu wa ndani wapewe elimu inayotosha lakini pia tuangalie kama wanaweza wakawa kwa njia moja au nyingine wanashirikiana pengine na wahasibu wa kawaida katika kuiba pesa za Serikali.

Lakini lililo muhimu zaidi, mimi nadhani kuwe na uwajibikaji sasa. Pesa zaidi ya Shilingi milioni 700 zinapopotea kwenye Taasisi, lakini wakubwa wa sehemu zile wanabaki wako tu salama na hakuna hatua zinazochukuliwa, mimi nadhani na wenyewe ni utaratibu ambao sio mzuri.

Mheshimiwa Spika, nimewahi kupata taarifa nadhani sio ngeni kwa Watanzania wote, mwaka 1976 Rais wa Awamu ya Pili, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu, alikuwa Waziri wa Mambo ya Ndani wakati huo. Kuna mauwaji yalitokea Mkoani Shinyanga. Sasa kwa sababu yeye alikuwa Waziri wa Mambo ya Ndani na hakuwepo kwenye eneo hilo, lakini alilazimika kujiuzulu kwa sababu tu ya *answerability.*

Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba, ili kujenga pengine nidhamu ya kazi, wakubwa wanaohusika kwenye maeneo kunapotokea na wizi na upotevu mkubwa sana wa fedha na mali za Serikali, basi na wenyewe wachukuliwe hatua. *(Makofi)*

Kwa sababu inawezekana hata wakubwa hao wanakula njama na wadogo, lakini wadogo wanakuwa chambo na kwa sababu wao wanajua kwamba hawawezi kuguswa katika matukio kama haya. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba sana niishauri sana Serikali na pengine kama hii isingekuwa Serikali mpya, ungeweza hata kuwaambia Wabunge tuwaambie hata Serikali waangalie namna ya baadhi ya fedha hizi zinavyoweza kurejeshwa kwa sababu kuna njia kabisa ya fedha hizi kuweza kurudishwa.

Mahali pengine tutaona kwamba, kesi zinaendelea. Hivi mimi nilikuwa najiuliza, kesi ilikuwa inaendelea miaka minne, miaka mitano, miaka sita, tuna viongozi wetu wa Serikali, tuna Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wanafanya *intervension* gani au wanafuatilia kiasi gani pale ambapo kesi ya wizi wa fedha au mali za Serikali inapotokea kwa muda wa miaka minne, miaka mitano kesi ipo Mahakamani? Wao kama Serikali wanachukua hatua gani?

Mheshimiwa Spika, mimi hilo lilikuwa kwa kweli kupitia taarifa hii imenigusa sana. Kama nilivyosema, lingehitaji mtu utulie kuisoma taarifa hii vizuri ili tuweze kuishauri Serikali ili iweze kuwa makini katika mali zake na pesa za Serikali. Tunajua wote kwamba hizi ni pesa za walipakodi, ni pesa za Watanzania wengine walio maskini sana. Wanaposikia pesa zinapotea na kuibiwa katika mazingira ya kutatanisha, hili linawasononesha na kuwakatisha tamaa sana kuendelea pengine kuchangishwa ili kupata maendeleo au kwa ajili ya shughuli mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba basi, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ayatolee maelezo haya kwa nini wizi wa namna hii unatokea hatuelezwi hatua muhimu zinazochukuliwa? Kwa sababu tukiacha hivi hivi, yataendelea kutokea na baadaye taarifa hizi zitakuwa zinaletewa mbele ya Bunge kwamba Waziri anaomba sasa tumpe nguvu za kuweza kufuta madeni haya. Itakuwa ni kitu cha kawaida!

Kwa hiyo, sisi tunaomba kwamba kwa sababu tunaamini kwamba ni Serikali mpya, basi na Bunge likubali lakini tusikubali taarifa kama hizi kwa miaka mingine inayokuja. Hata Bunge lenyewe litaonekana sasa haliwezi kufanya kazi sawasawa ya kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, mimi naomba nimalize kwa kutoa tu ushauri kwa Serikali kama nilivyosema iwe makini sana katika kuchukua taarifa

au hatua za mapema ili kuweza kukabiliana na upotevu wa fedha pamoja na vifaa vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja hii ya Azimio la Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kwanza kabisa, napenda kuunga mkono azimio hili, kwa sababu zifuatazo:-

Tukumbuke kwamba, Serikali haianzi leo, ni mwendelezo wa awamu za Serikali. Kwa hiyo, Bunge lililopita lilitoa ushauri na maelekezo kwa Serikali kwamba wakati Waziri anapoleta hoja ya kufuta upotevu, basi alete mchanganuo wa kina.

Mimi napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Serikali kwamba wametekeleza maelekezo na ushauri wa Wabunge. Hilo ni moja.

Mheshimiwa Spika, kama mtu amesoma vizuri taarifa hii, mimi kidogo imenipa taabu moja tu, kwamba, hili jalada lake la juu limepambwa na nembo ya Taifa, *the Court of Arms* na bendera. Mimi nashauri vitu hivi viovu visipambwe na bendera ya Taifa na nembo namna hiyo. Iachwe tu hivyo hivyo, maana yake inapendeza kwa kweli, lakini ukisoma sasa unakuta ni madudu haya. Mimi ndiyo nilivyoona hivyo, nadhani isipambwe kiasi hicho. Haileti hisia nzuri. Ukiipata hii utavutiwa sana kwamba ni kitu kizuri kumbe ndani humu ni upotevu na kadhalika. Haya ni maoni yangu mimi binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kufanyike sahihisho kwenye Jedwali ambalo halina namba, lile linaloanza baada ya karatasi ya kwanza pale kwenye Fungu Na. 42, *Vote 42* ningeomba pale iandikwe Ofisi ya Bunge na siyo Spika wa Bunge. Ukiandika Spika wa Bunge, maana yake ni yeye Spika ndiye aliyehusika na upotevu huo. Lakini kwenye Jedwali linalofuata imeandikwa vizuri Fungu 42 ni Ofisi ya Bunge. Hilo sahihisho nadhani ni muhimu, vinginevyo Spika ataonekana ndiyo yeye ambaye amepoteza, amefanya upotevu huo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ufafanuzi huu kusaidia wenzetu wa Upinzani kwamba, hizi taarifa ni vizuri wazisome kwa kina. Kwa sababu kama umesoma vizuri hii taarifa siyo ya mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2005. Hii taarifa inahusu matukio ya huko, wakati wa miaka iliyopita. Kwa mfano, hii inayozungumzia Ofisi ya Bunge, upotevu mmoja umetokea tarehe 1 Oktoba, 1990. Halafu ule upotevu wa vifaa umetokea katika mwaka wa fedha 1990/1991, wakati huo Ofisi ya Bunge ndiyo ilikuwa inashughulikia Fungu la Uchaguzi.

Kwa hiyo, tunapoisoma hii tusifikirie ni ya mwaka mmoja hii. Ni ya miaka mingi kurudi nyuma huko na ni maelekezo ya Bunge kwamba sasa Waziri atazame hali yote atuletee hapa asituletee vitu vichache vichache hivi. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Zambi, kwamba, hapa tunaanza upya sasa. Tufunge hii tumkubalie Waziri afute hayo. Sasa yakitokea mengine, sasa itakuwa watu kwa kweli wawajibike. Kwa

mfano ukitaka kumwajibisha mtu aliyekuwepo mwaka 1990 na 1991 utapoteza muda wako na hata kama ni kuchukua hatua sijui utamchukulia nani na yuko wapi huyo mtu.

Mheshimiwa Spika, nadhani kwa kuwa mambo haya yanafanyika hata kwenye biashara binafsi, kwamba kama umeshindwa kupata mapato uliyofikiria kupata, basi lazima ufute hiyo ili vitabu vyako visichafuke na ndicho kinachofanyika hapa na ndiyo utaratibu unaofanyika huo. Kwa hiyo, mimi sioni ajabu. Lakini faraja yangu iko kwamba baada ya kufanya mchanganuo, nimekuta asilimia 96 ni maduhuli ambayo hayakukusanywa.

Kwa hiyo, hakuna mtu aliyekula fedha hapa. Maduhuli hayakukusanywa isipokuwa labda kumekuwa na uzembe au kutokuwa na ufanisi wa kutosha. Ni vizuri tukakubaliana hilo ili isije ikaandikwa kwamba Shilingi hizi zote karibu bilioni 47 mmeziweka kwenye namba ambayo inasomeka vizuri. Shilingi bilioni 47 zote ni wizi umefanyika, hapana. Asilimia 96 au Shilingi bilioni 45 ilikuwa ni maduhuli ambayo haikukusanywa. Sasa kama kuna uwajibikaji itabidi kurudi mpaka mwaka 1991 huko nyuma.

Sasa hiyo nadhani ni kazi ambayo ningeomba tusimpe Mheshimiwa Meghji, Waziri Meghji tumpe sasa kuanzia sasa yasitokee mengine kama haya. *(Makofi)*

Lingine la mwisho, nilikuwa nataka kupendekeza kwamba kwa sababu haya kwa kweli ndio mambo ambayo yanaudhi kweli wananchi na kadhalika na inabidi kwa kweli iangaliwe kwa kina.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri sasa utekelezaji unaokuja tuelezwe kwamba aliyehusika ni fulani kwa yale ambayo ni karibu. Yale ya mwaka 1991 tunapoteza muda. Hatua gani Serikali imechukua kwa maana, nikiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Zambi ya uwajibishaji wa watu ambao wanahusika na haya ili tutoe fundisho na hesabu zetu ziwe nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba wenzangu tushirikiane, tuunge mkono azimio hili, tufute hayo, lakini tuweke misingi mizuri ya huko tunakokwenda na wenzangu wa Upinzani, ninaomba twende na wakati. Huku kung'ang'ania ng'ang'ania vitu hivi, sasa hukubali yafutwe maana yake nini? Vitabu viendelee kuharibika?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Nimekumbushwa kwamba kumbe Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alikuwa ameleta jina lake hapa kuchangia, kufafanua baadhi ya mambo yanayohusiana na Azimio hili. Kwa hiyo, sasa nampa nafasi.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kutoa mchango wangu mdogo katika hoja hii. Kwanza, napenda kusema wazi kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja hii inahusu sana matumizi ya Serikali na usimamiaji wa fedha ndani ya Serikali. Nilipenda niseme kidogo kuhusu namna tunavyojitahidi kusimamia ili tusiwe tunajikuta na matokeo ya aina hii ya kulazimika kufuta hasa katika eneo ninalolisimamia. Kuna jambo lilizungumzwa hapa Bungeni, nikaona kama Mheshimiwa Mbunge mwenzangu mmoja hakuelewa hatua ambayo ilichukuliwa na Serikali na mimi mwenyewe nikawa nahusika moja kwa moja kuchukua hatua ya haraka kwenda kusimamia.

Mheshimiwa Spika, tukiwa hapa Bungeni, wakati wa kipindi hiki cha Bajeti, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitembelea Mkoa wa Mtwara kwenda kuona mradi maalum kwa shughuli maalum na alikwenda katika kipindi cha mapumziko ya mwisho wa wiki *(weekend).* Alipofika kule Mtwara katika vijiji viwili Mheshimiwa Waziri Mkuu alishikiwa mabango, wananchi walishika mabango ya malalamiko kuhusu uhaba ama uchache wa dawa za korosho hususan dawa ya *sulphur* ambayo wakulima wanaihitaji sana na tuliwaahidi kwamba wataipata.

Mheshimiwa Waziri Mkuu aliporudi akaniagiza mimi kama Waziri ninayesimamia sekta hiyo, niende haraka. Kwa hiyo, nikaenda mara moja kule Mtwara nikafanya kazi kwa muda wa siku tatu, kufuatilia yale matatizo. Nikaenda mpaka kwenye vile vijiji walikoshika yale mabango. Sasa Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo alipokuwa anachangia hapa Bungeni alipokuwa anachangia hoja ya Sheria ya Fedha, alisema kwamba mimi nilikwenda Mtwara kwa kulazimishwa tu na Waziri Mkuu, la sivyo sipendi kwenda. Sasa nilikuwa napenda nichukue nafasi hii kufafanua kwamba Waziri Mkuu ndiye Kiongozi wetu Mawaziri. Anapokuta matatizo mahali, ana tabia ya kutuagiza twende haraka. *(Makofi)*

Kwa kufanya hivyo, ningependa ieleweke kwamba, ni kwenda kusimamia kwa sababu katika jambo hili tulikuwa na programu na *subsidy* ya korosho. Kwa hiyo, Waziri Mkuu alishtuka kwamba fedha tumetenga tumekaa katika vikao, tumekubaliana; kwa nini wananchi hawa washike mabango? Fedha hizo zimekwenda wapi? Kwa nini korosho haipo na hali tulitenga fedha.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu akaagiza niende mara moja. Kwa hiyo, napenda Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo aelewe kwamba hii ni mojawapo ya hatua ambazo zinachukuliwa na Serikali. Tunaposikia tatizo lipo mahali, ni mhusika mkuu kusimamia akiagiza kwenda haraka isichukuliwe *negatively* kwamba amelazimishwa tu.

Kwa hiyo, nilipenda nichukue nafasi hii nilieleze na katika mchango wake huo, alidai kwamba, alionyesha hisia kwamba labda mimi silipendi zao la korosho au siipendi Mikoa inayolima korosho. Kwa hiyo, napenda nichukue nafasi hii kufafanua. *(Makofi)*

Niseme nitakuwa Waziri wa Kilimo wa ajabu kabisa kama nitapuuza mmoja wa mazao muhimu ya kilimo ya biashara katika nchi yetu. Kwa hiyo, nilikuwa napenda nifafanue kwa Mbunge mwenzangu asije akanielewa vibaya kwamba sipendi zao la korosho, sitaki kwenda Mtwara.

Nilipenda nichukue nafasi hii pia nieleze kwamba yale maelezo niliyoyatoa kwenye Kamati yetu tulipokaa Wabunge wote kwamba mpango wa korosho tunauandaa, sikuwa nasema kwa kupuuza. Inaelekea sikueleweka pale, ikadhaniwa kwamba ninakwenda.

Nilipokuwa nazungumzia ruzuku ya mbolea na mbegu, napenda nimhakikishie kwamba baadhi ya maandalizi ambayo Serikali inafanya ni pamoja na hiki kilichojitokeza katika Sheria ya Fedha, kwamba katika asilimia 10 ya *Export leavy* iliyotengwa kwenye korosho asimilia 6.5 inaelekezwa moja kwa moja kwenye Wilaya zinazolima korosho na hizi ni fedha ambazo niliposema tutaandaa mpango ni sehemu ya fedha ambazo tutaziweka katika Bajeti.

Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba, nilipokuwa natoa yale maelezo *Finance Bill* ilikuwa haijapitishwa, sasa *Finance Bill* imepitishwa na Waziri mwenzangu wa fedha, ameshatoa maelekezo kuhusu hii asilimia 6.5, waraka umeshatoka Hazina kwamba kule Wilaya uelekezwe kwenda kwa ajili ya zao la korosho.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mwongozo wa Spika.

Mheshimiwa Spika, kanuni ya 50(2) kila Mbunge atasemea lile jambo ambalo liko katika mjadala tu. Pamoja na mazungumzo mazuri sana na maelezo mazuri sana ambayo Mheshimiwa Waziri anayazungumza, lakini hoja ya Mheshimiwa Njwayo, ilikuwa ni katika sheria ya fedha ambayo jana tumekwishaifanyia uamuzi na sasa hivi tunazungumzia suala la Azimio la Kufuta Madeni. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri anaongea jambo ambalo tayari Bunge limeshafanyiwa uamuzi. Naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, nadhani hilo alilosema Mheshimiwa Zitto, kwa kiasi Fulani ni kweli ningemuomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, sasa amalizie pale alipofikia, ili tufunge hili jambo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nimalizie, labda katika kueleza jambo hili la matumizi ya fedha.

Nimejikuta nimechepuka kidogo, nimekwenda kwenye kuelezea *program*, lakini nilichotaka kufafanua hapa ni kwamba, katika kusimamia matumizi ni pamoja na hatua zinazobidi zichukuliwe haraka na Mawaziri, kwenda kule kwenye matatizo na kwa mfano sasa hivi imeibuka jambo limezungumzwa hapa moja ya mambo makubwa yamezungumzwa ni matatizo ya Mbarali na kadhalika na tarehe 18 nitakuwa Mbarali kwenda kusimamia kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naungana hoja mkono na Mheshimiwa Zitto. Ahsante kwa kunirudisha kwenye *line*. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (ABDISALAAM I. KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Kwanza, nawashukuru Waheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Shellukindo, Mheshimiwa Zambi na Mheshimiwa Manyanya ambaye ameleta kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Shellukindo, amenisadia sana kufafanua madhumuni ya Azimio hili. Napenda nirudie tena, kama nilivyosema wakati natoa Azimio hili, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba kufutwa kwa hasara hii hakumaanishi Serikali iliwasamehe wadeni hawa, bali itaendelea kufuatilia kupitia taratibu za kisheria. Ikiwa pamoja na kuhakikishia kesi iliyofunguliwa na Wizara ya Ujenzi Mahakamani, inaendelea hadi hukumu itakapotolewa.

La pili, kama alivyofafanua Mheshimiwa Shellukindo, upotevu huu ukiangalia, umeanza kuanzia mwaka 1981 *trio* ya 2000 *and* 2004/2005, sio wakati mmoja na utaona kwamba hasa hicho kilichopotea ambayo tumekosa kwamba ni mapato ya Serikali, ni bilioni 1.7 kilichobakia hizo asilimia 96 ya Mheshimiwa mtoa hoja upande wa wapinzani amesema ile ilikuwa maduhuli ambayo haikupatikana na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lililopita kwamba hapo zamani Waziri wa Fedha alikuwa ni yeye tu anaye *write off* huu upotevu.

Bunge likasema sasa upotevu usiwe unaletwa hapa tu kufuta kama sisi labda ni *rubber stamp*, lazima lije Azimio la Bunge kufuta upotevu wa aina hii. Ikumbukwe kwamba siku zote hata ukiwa umefika hapo, *PS* imekuwa ikiangalia na kuyapitia na kuyarudisha haya kafaidika. Kafanyeni kazi na baada ya hapo hapa tunasema tena lazima tufute katika madaftari yetu ndilo tunaloomba kwenu Waheshimiwa Wabunge.

Kulikuwa na hoja ya *TANESCO*, *TAZARA*, kwanini wafutiwe madeni hayo? *TAZARA*, *TANESCO* na *TFC* walikuwa hawakulipa *payee in time* sio kwamba *payee* hawakulipa kwa wakati, kwa hiyo, hii tunaifuta ni ile faini ambayo tumewatoza wao lakini kwa sababu hawana uwezo kwa sasa, tukasema tuyafute yasiwemo katika madaftari yetu. Hii ndio maana yake.

Tunachukua hatua gani? Katika juhudi za kudhibiti hasara za namna hii zisitokee, Serikali itatumia sheria ya fedha na sheria za manunuzi na kanuni zake kwa maeneo yafuatayo:-

Kwanza kuwa na mpango maalum wa ununuzi, yaani *procurement plan*. Hii itaondoa uwezekano wa kuwa na mali zilizopitwa na wakati au zisizohitajika. Vilevile, Serikali kwamba imejiondoa katika biashara ya madawa za pembejeo, ilitusaidia vilevile.

Tutakuwa na *performance both* kwenye mikataba ya ununuzi, tutawafungia wazabuni wakorofi, *break list* hatuwaruhusu kabisa, kuwa na Bodi ya Uchunguzi ya Kudumu, kulipia mishahara ya watumishi kupitia mabenki na kutumia mabenki kupokea na kukusanya maduhuli.

Hata hivyo, ushauri wa *PAC* na ushauri mliotoa Waheshimiwa Wabunge, vilevile tutauzingatia ili kuboresha hali hii isiwepo huko tunakokwenda.
Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa ufafanuzi huo naomba kutoa hoja.

**MHE. HAMAD R. MOHAMED:** Mwongozo wa Spika.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 50(3): "Ni marufuku kwa Mbunge yoyote kuzungumzia jambo lolote ambalo linangojea uamuzi wa Mahakama, au jambo lolote lililohitaji na Mkutano uliopita." Lakini nazungumzia hii ya Mahakama tu.

Mheshimiwa Spika, katika hayo mapendekezo ya Mheshimiwa Waziri, aliyoleta jana, alituambia kwamba kuna kesi ya *KJ Motors* na nyingine ziko Mahakamani. Ni vipi Bunge linaweza kutoa maamuzi kwa jambo ambalo liko Mahakamani? Nataka ufafanuzi wako.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu cha 50 au kanuni 50(3) aliyoisoma Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, inahusu kuyazungumzia maudhui ya kile kilichopo Mahakamani, maudhui yake.

Hapa Bunge linachofanya ni kutekeleza wajibu wa kiufundi katika uhasibu kufuta upotevu, bila hata kuingilia kesi iliyoko Mahakamani. Kwa sababu kibaya hapa kwa Bunge ingekuwa ni kuzungumzia nani alipoteza alifanya nini, aligushi ama vitu kama hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, kilichopo mbele yetu hapa, ni kukiri kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Fedha, upotevu kama huu unabidi upitishwe na kukubaliwa na Bunge ili Waziri wa Fedha aweze kufuta na kufuta huko hakuhusiani hata kidogo na maudhui kwa maana ya kwamba tukio lenyewe halizungumzwi kabisa na Bunge. Ninaona Serikali na sisi sote tumelifuata hilo, kwa hiyo, hakuna athari yoyote.

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wangu ni kwamba, sasa tuingie katika kulipitisha hili Azimio ambapo nitawahoji. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

***Azimio la Kumwezesha Waziri wa Fedha Kufuta ama Kusamehe Madeni au Hasara Itakanayo na Upotevu wa Fedha au Vifaa vya Serikali***

*(Hoja ilitolewa iamuliwa)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Azimio la Kufuta au Kusamehe Madeni au Hasara Itokanayo na Upotevu wa Fedha au Vifaa vya Serikali liliadhimiwa na Bunge)*

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa kanuni 27(2) na utaratibu huu nitaufuata kila Bunge la Bajeti, kutoa taarifa fupi ya matukio muhimu ya Bunge la Bajeti.

Waheshimiwa Wabunge, tumekuwapo hapa Dodoma Bungeni kwa siku 65 kwa ajili ya Mkutano wetu huu wa kwanza wa Bajeti wa Bunge la 2005 – 2010.

Nimeona ni vyema nitoe taarifa fupi kwa Bunge kuhusiana na mambo muhimu yaliyojitokeza katika Mkutano wetu na pia kutaarifu kuhusu mambo machache ya baadaye.

Hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa Rehema na Baraka zake kwetu ambazo zimetuwezesha kuifikia na kuiona siku ya leo. Aidha, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mkubwa mlionipa wakati wote wa shughuli za Mkutano wa Nne wa Bunge hili la Bajeti.

Kwa namna ya pekee, nawashukuru sana Naibu Spika Mheshimiwa Anne S. Makinda na Wenyeviti wa Bunge - Mheshimiwa Job Y. Ndugai na Mheshimiwa Jenista J. Mhagama kwa msaada wao mkubwa wa kuendesha shughuli za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, sina shaka tutakubaliana kwamba uamuzi wetu wa kuwachagua Waheshimiwa hao kunisaidia humu Bungeni ulikuwa sahihi kwa vigezo vyovyote.

Aidha, nachukua nafasi hii nimshukuru kwa nguvu zote Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa na timu yote ya Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa ufanisi na umahiri mkubwa wa kazi zao zilizozingatia na kutujali sisi Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge,uhai wa Bunge, yaani miaka mitano, huwa una mikutano ishirini (20). Kama mlivyokuwa mkiona kwenye Orodha ya Shughuli za kila siku, ilikuwa inaandikwa juu ya hiyo Orodha ya Shughuli Mkutano wa Nne, hivyo bado tuna Mikutano 16 iliyo mbele yetu. Tutaendelea kuziomba baraka za Mungu ili awe pamoja nasi hadi mwisho. *(Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Mkutano wa Nne wa Bunge ulikuwa Mkutano wa Kwanza mrefu tangu Bunge la Awamu ya Nne lianze kazi mwishoni mwa mwezi Desemba, 2005. Nikiwa Spika wa Bunge, Mkutano huu umenipa fursa ya kujifunza na kupata uzoefu zaidi juu ya uendeshaji wa shughuli za Bunge.

Aidha, Mkutano huu pia umeniwezesha kuwafahamu Waheshimiwa Wabunge mmoja mmoja na hivyo kurahisisha kazi zangu za Uspika. Vile vile, katika kipindi hiki

kirefu, tumeweza kujenga maelewano na ushirikiano miongoni mwetu na hivyo kujihisi kuwa ni familia moja yenye malengo na dhamira zinazoshabihiana. Nina hakika kuwa wengi wenu pia Mkutano huu mrefu umekuwa ni jukwaa la mafunzo kuhusu masuala mbalimbali ya Kibunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunapofikia mwisho wa shughuli za Mkutano wa Nne wa Bunge, nimeona ni busara nikiwa Spika na Kiongozi wa Bunge nitoe taarifa kwenu japo kwa kifupi kuhusu shughuli mbalimbali tulizozitekeleza wakati wa Mkutano wa nne wa Bunge. Aidha, wasaa huu pia utaniwezesha kueleza masuala muhimu yaliyojitokeza pamoja na hatua ninazokusudia kuchukua ili kuboresha utendaji wa shughuli za Bunge.

Kwanza, Shughuli za Bunge, Bajeti ya Serikali, napenda kuwaarifu kuwa shughuli zote za Bunge zilizopangwa kutekelezwa katika Mkutano wa Nne zimekamilika kama ilivyopangwa. Kama mjuavyo, Mkutano huu ulikuwa ni Mkutano wa Bunge la Bajeti.

Hivyo, Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali zimewasilisha Makadirio ya Matumizi ambayo yaliidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977). Naamini kuwa michango mbalimbali mliyoitoa wakati wa majadiliano ya Bajeti itazingatiwa na Serikali ili kuwaletea wananchi wetu ustawi wa jamii na maendeleo ya kiuchumi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mojawapo ya njia muhimu ambazo huliwezesha Bunge kusimamia na kuishauri Serikali ni kupitia maswali yanayoulizwa na Waheshimiwa Wabunge. Katika Mkutano wa Nne, jumla ya maswali 415 yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kupata majibu ya Serikali.

Aidha, nafurahi kuona kuwa Waheshimiwa Wabunge wengi wameridhishwa na majibu yaliyotolewa na Serikali. Nadhani wengi wenu mtakubaliana nami kwamba kiwango cha majibu ya Serikali kwa ujumla kimekuwa ni cha hali ya juu kuliko ilivyokuwa katika miaka iliyopita. Kumekuwepo utafiti wa kina kwa kila swali na hivyo majibu yamekuwa yasiyo na ubabaishaji au yanayokwepesha ukweli.

Nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kazi yao safi sana ambayo imeimarisha hadhi ya Bunge letu miongoni mwa jamii.

Waheshimiwa Wabunge, Miswada ya Sheria iliyosomwa mara ya kwanza, Bunge ni Chombo cha kutunga sheria zinazosimamia utekelezaji wa sera mbalimbali pamoja na kulinda haki za binadamu. Katika Mkutano wa Bunge la Bajeti unaomalizika, Miswada ifuatayo ya Sheria imesomwa kwa mara ya kwanza:-

(i) Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2006;

(ii) Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu wa mwaka 2006;

(iii) Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho kwenye Sheria mbalimbali wa mwaka 2006; na

(iv) Muswada wa Sheria ya kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali za Serikali za Mitaa wa mwaka 2006.

Naelewa kwamba Waheshimiwa Wabunge mmekwishapatiwa nakala za Miswada hiyo ya Sheria ili mtakapokwenda Majimboni muweze kuwashirikisha wananchi kwa kupata maoni yao kuhusu maudhui ya Miswada hiyo ya sheria.

Waheshimiwa Wabunge, Miswada ya Sheria ya Serikali iliyopitishwa katika hatua zote, sanjari na kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2006/2007 Bunge pia limepitisha Miswada miwili ya Sheria ifuatayo:

(1) Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2006 *(The appropriation Bill, 2006);* na

(2) Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2006 *(The Finance Bill, 2006).*

Waheshimiwa Wabunge, Maazimio yaliyoridhiwa na Bunge Katika Mkutano huu wa Nne, Bunge limeridhia Maazimio yafuatayo:-

(i) Azimio la Bunge Kuhusu Kulaani Filamu chafu iitwayo *Darwin's Nightmare;* na

(ii) Azimio la Kumwezesha Waziri wa Fedha kufuta na kusamehe madai au hasara itokanayo na upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, masuala yaliyopelekwa na Mheshimiwa Spika Kwenye Kamati za Bunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 88(9) Toleo la 2004, Mheshimiwa Spika anayo mamlaka ya kuipelekea Kamati yoyote ya Kudumu ya Bunge jambo lolote ili Kamati ilishughulikie kama atakavyoona inafaa. Hivyo, kwa kuzingatia masharti ya kanuni hiyo, nilipeleka masuala yafuatayo kwenye Kamati za Kudumu za Bunge ili zifanye uchunguzi na hatimaye kuwasilisha taarifa Bungeni.

Kwanza, kauli ya Mheshimiwa John M. Cheyo, kuwa Mheshimiwa John M. Shibuda alisema uwongo wakati akichangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula na Ushirika, suala hili nililipeleka kwenye Kamati ya Kilimo na Ardhi.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwaarifu kuwa Kamati hiyo tayari imekwishawasilisha taarifa yake kwangu na ninasubiri kutangaza maamuzi yangu katika wakati muafaka. Kwa hakika ningetangaza ila Mheshimiwa John M. Cheyo, hajakuwepo kwa zaidi ya wiki moja na sio haki kutangaza wakati hayupo.

Pili, kauli ya Mheshimiwa Chaha Z. Wangwe kwamba wananchi kadhaa waliuawa huko Tarime na Maofisa wa Jeshi la Polisi kwa misingi ya Kisiasa, suala hili lilipelekwa kwenye Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama. Bado sijapokea ushauri wa Kamati.

Tatu, malalamiko ya *IPP Media* dhidi ya Mheshimiwa Adam Malima kwamba hakuwatendea haki *ITV* wakati akichangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo; aidha, malalamiko ya Mheshimiwa Malima kutaka mwongozo wa Spika kwa kuona kwamba taarifa za *ITV* zilizofuatia hotuba yake zilimdhalilisha; hoja hzi zilipelekwa kwenye Kamati ya Bunge ya Haki Maadili na Madaraka ya Bunge ili kumsaidia kupata ushauri na hatimaye niweze kutoa uamuzi.

Waheshimiwa Wabunge, pia katika kipindi hiki, nimetoa miongozi mbalimbali mifano yake ambayo tutaiona katika hotuba hii ambayo itagawiwa baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano huu tukikaa kama Kamati, tulipitisha Makadirio mbalimbali lakini pia tulilazimika kupitisha kwa mafungu Makadirio ya Wizara kama vile Wizara ya Miundombinu, Kilimo Chakula na kadhalika, kwa sababu ya kukosa muda.

Aidha, katika Mkutano huu, niliwakumbusha Waheshimiwa Mawaziri kwamba, unapofika muda wa kujumuisha hoja za Wabunge, wasijumuishe tu yale yaliyochangiwa na Wabunge kwenye Wizara zao, lakini pia wazingatie yaliyokwishasemwa kwenye hotuba za Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri Mkuu, utaratibu ambao ulifuatwa na wote tulipata majibu.

Waheshimiwa Wabunge, hadi Mkutano huu, hapakuwa na utaratibu wa Spika kutengewa Kiti ndani ya Ukumbi wa Bunge kwa ajili ya kukitumia endapo atapenda kufanya hivyo. Lakini sasa utaratibu huo umewekwa na sasa Spika ametengewa Kiti chake ndani ya Ukumbi wa Bunge japokuwa wakati amekikalia hawezi kuchangia hoja au kuuliza swali. Kiti hicho kilianza kutumiwa kuanzia tarehe 19 Julai, 2006.

Natambua yalitolewa maelezo binafsi na Mheshimiwa Charles Kajege chini ya Kanuni ya 21(9) kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwamba sehemu ya mchango kwenye Bajeti ya Wizara hiyo, haikuwa sahihi kutokana na kupewa maelezo ambayo baadhi yake hayakuwa na ukweli. Wabunge walitakiwa mara kwa mara kufuta kauli zao ama na Spika au Mbunge mwingine yeyote ambazo hazikuwa na usahihi. Walipotakiwa kufanya hivyo, walifuta kauli zao ambazo hazikuwa sahihi na wote walipotakiwa kufanya hivyo walitekeleza pale ambapo hazikuwa sahihi.

Waheshimiwa Wabunge, ufanisi wa uendeshaji wa Shughuli za Bunge unategemea kwa kiasi kikubwa mazingira bora ya uendeshaji wa shughuli hizo. Kwa mantiki hiyo, hatua mbalimbali zimechukuliwa na zitaendelea kuchukuliwa ili kuliwezesha Bunge kuwa na mazingira bora na tulivu ya kuifanya kazi.

Waheshimiwa Wabunge, Mkutano huu unaomalizika, umeshuhudia mafanikio yafuatayo:-

Kwanza, uzinduzi wa Ukumbi Mpya wa Kisasa wa Bunge, ambao ndio huu tunautumia. *(Makofi)*

Pili, kuanza mchakato wa Marekebisho ya Kanuni za Bunge. Kama mnavyofahamu, niliteua Kamati Maalum ili kuzipitia upya Kanuni zetu na kupendekeza maeneo yanayohitaji marekebisho au kuongezwa ili kuleta ufanisi katika uendeshaji wa shughuli za Bunge. Wajumbe wa Kamati hiyo maalum ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mwenyekiti; Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Nimrod E. Mkono *(Makofi)*

Napenda kuwaaarifu kuwa, Kamati hiyo imekwishawasilisha taarifa yake katika randama *(volume)* III. Aidha, nimetuma nakala za taarifa hiyo kwa Serikalini ili kwa pamoja tuweze kuzipitia kwenye Mkutano wa Tano wa Bunge. Ni imani yangu kuwa tutaweza kutoa toleo jipya la Kanuni za Bunge wakati wa Mkutano wa Tano wa Bunge kwa kuyaafiki yale mabadiliko ya Kanuni yatakayokubalika na pande zote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niliwaomba pia Waheshimiwa Mawaziri watoe majibu kwa maandishi kwa kukusanya majibu hayo katika makala ambazo tutagawiwa sote. Mantiki ya ombi hili ni kutuwezesha kuwa na ufahamu unaolingana katika masuala mbalimbali ya nchi yetu. Utaratibu ulivyo sasa ni kwamba, majibu hutolewa kwa mwuliza swali au mtoa hoja tu. Naamini kuwa tukirekebisha hali hii itatuwezesha Wabunge kujifunza uzoefu wa Majimbo mengine na pia kuwa na ulinganifu wa utekelezaji wa sera kwa sekta mbalimbali na maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Waheshimiwa Wabunge, Wakati wa Mkutano wa Nne wa Bunge takribani jumla ya Waheshimiwa Wabunge 50 walipata fursa ya kusafiri nje ya nchi kikazi. Mikutano, Warsha na ziara za Wabunge nchi za nje ni njia mojawapo ya kuwajengea uwezo Waheshimiwa Wabunge ili waweze kutekeleza kazi zao za Kibunge kwa ufanisi.

Aidha, ziara hizo hutoa fursa ya kubadilishana uzoefu, mawazo na kujifunza masuala mbalimbali kutoka kwa Wabunge wenzao wa nchi nyingine. Nafurahi kuwaarifu kuwa Ofisi yangu imekwishatayarisha Ziara za Mafunzo kwa wabunge 90 zinazotarajiwa kufanyika kuanzia sasa hadi Oktoba, 2006. Aidha, hatua zaidi zitachukuliwa ili kuhakikisha kuwa Waheshimiwa Wabunge wote wanapata fursa hizo kwa awamu katika siku zijazo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mkutano wa Nne wa Bunge ulishuhudia matukio muhimu yafuatayo:-

- Uzinduzi wa Ukumbi huu, tukio hili lilishuhudiwa na Viongozi mbalimbali mashuhuri wa Kitaifa.

- Kuapishwa kwa Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba kuwa Mbunge mnamo tarehe 20 Juni, 2006 baada ya kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge kwa mujibu wa Katiba. *(Makofi)*

- Bunge letu kutembelewa na kuhutubiwa na Rais wa Ireland Mheshimiwa Dr. Mary Mc Aleese tarehe 22 Juni, 2006. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Matazamio, Dira (*Vision*) ya Ofisi Bunge inalenga katika kujenga Taasisi ya Bunge ambayo ni ya kuigwa kwa ubora *(model of excellency)* iliyo karibu na jamii *(accessible to the public)* na inayokuza demokrasia *(enhance democracy)*, ndani ya Bunge na ndani ya nchi yetu.

Waheshimiwa Wabunge, nafurahi kuwafahamisha kwamba mchakato umeanza wa kujadiliana na Serikali ili tukubaliane kuhusu mambo muhimu yafuatayo:-

(i) Kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo. Utaratibu huu umeonyesha mafanikio makubwa katika nchi kadhaa pamoja na nchi majirani zetu. Waraka rasmi unaandaliwa na Ofisi ya Bunge ili kuifikisha Serikalini. Lengo ni kwamba, utaratibu huo uweze kuanzishwa mnamo mwaka wa fedha ujao 2007/2008. *(Makofi)*

(ii) Bunge kuwa na Bajeti inayojitegemea ya moja kwa moja kutoka Mfuko Mkuu wa Fedha (*Consolidated Fund*). Chini ya utaratibu huo itawezekana Bunge kuwa na uhuru zaidi wa mipango na matumizi yake kwa mfumo na kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria ya Tume ya Huduma za Bunge ya mwaka 1997. *(Makofi)*

(iii) Pamoja na pendekezo hilo nililolitaja, Ofisi ya Bunge itapendekeza kuhamishia jukumu la ujenzi na uendeshaji wa Ofisi za Wabunge zihamie Ofisi ya Spika. Uzoefu umeonesha kwamba, sio rahisi kwa Ofisi ya *DC* kutoa kipaumbele kwa masuala ya Ofisi za Wabunge. Hata kwa mfumo huu tu, huduma zote za Mbunge husimamiwa na Ofisi ya Bunge na ingestahili hata suala la Ofisi za Wabunge, nalo lisimamiwe na Ofisi ya Bunge. *(Makofi)*

(iv) Pamoja na hayo, tunayo matumaini makubwa kwamba, Serikali italikubali ombi la Bunge kuwashirikisha Wabunge kwenye mchakato wa kupanga Bajeti kwa kuitisha Kikao maalum cha Kamati ya Bunge Zima mnamo mwezi Januari kila mwaka ili Bunge liweze kutoa maoni yake kuhusu mwelekeo wa Bajeti.

Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba utaratibu huo unaweza ukapangwa ili uanze katika mwaka wa fedha 2007/2008. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matumaini makubwa kwamba tutafikia muafaka na Serikali kuhusu mapendekezo haya niliyoyataja ambayo naamini wakati wake umefika.

Waheshimiwa Wabunge, mwisho, napenda kuhitimisha taarifa yangu kwa kutoa shukrani.

Namshukuru kwa dhati Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutujali sisi Waheshimiwa Wabunge na kutupatia ushirikiano wa hali ya juu katika kufuatilia na kutafuta ufumbuzi wa matatizo yaliyoko Majimboni mwetu.

Aidha, namshuruku pia kwa kuiongoza Serikali kufanya kazi zake muda wote kwa umakini ambao unakidhi kwa dhati hoja za Wabunge. Tunamshukuru pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ufuatiliaji wake wa karibu ahadi za Serikali zinazotolewa humu Bungeni. *(Makofi)*

Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Uongozi na Makamishna wa Tume ya Huduma za Bunge kwa msaada wao wa karibu uliowezesha uendeshaji mzuri wa shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Tatu, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa uvumilifu na ustahimilivu wao, kwa kipindi chote cha takriban siku 65, ambazo hapa na pale yametokea makosa. Namshukuru Katibu wa Bunge na Wafanyakazi wa Ofisi ya Bunge, kwa kufanya kazi bila kujali muda wa kawaida wa saa za kazi. *(Makofi)*

Aidha, nawashukuru waandishi wa habari, kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuwaarifu wananchi juu ya shughuli za Bunge. Mwisho, nisiwasahau wenyeji wetu wa Dodoma, Viongozi na Raia wa kawaida wa Dodoma, ambao wametulea vyema katika kipindi chote tulipokuwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Sasa naomba kwa heshima na taadhima, nimkaribishe Mheshimiwa Waziri Mkuu, atoe hoja ya kuliahirisha Bunge. Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu. *(Makofi)*

## HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, tarehe 13 Juni, 2006 tulianza kikao cha kwanza cha Mkutano wa Nne wa Bunge lako Tukufu. Ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba, leo tunahitimisha shughuli zote zilizopangwa kwa amani na salama. Mkutano huu ulikuwa mahsusi kwa ajili ya kuwasilisha, kujadili na hatimaye kupitisha Bajeti ya Serikali, pamoja na Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara, Mikoa na Taasisi mbalimbali. Aidha, katika mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge, walipata fursa ya kuuliza jumla ya maswali 415 ya msingi pamoja na mengine mengi ya nyongeza, ambayo yalijibiwa na Serikali. Katika mkutano huu pia, Bunge lako Tukufu

lilipitisha Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2006 na Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge, kwa kutumia muda wote wa mkutano huu, kwa ufanisi mkubwa sana. Jambo ambalo limejitokeza na linalotia moyo ni jinsi Waheshimiwa Wabunge, walivyochangia kwa umakini, hoja zinazolenga kujenga na kusaidia Taifa letu. Wote mtakubaliana nami kwamba, mjadala ulikuwa wa kina, wenye kutoa msisimko na wa kiwango cha juu. Aidha, hoja zilijengwa katika ubora unaostahili. Kutokana na hali hiyo, iliwalazimu watoa hoja, kujiridhisha kwanza, kama wamejiandaa vizuri katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Kwangu mimi niliona kwamba, Waheshimiwa Wabunge walikuwa na hoja ambazo zililenga katika kujenga nchi yetu. Napenda kuchukua nafasi hii, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, kwa mwamko huo mzuri, ambao umetoa changamoto na msisimko mkubwa wakati wote wa kipindi cha majadiliano hapa Bungeni. Ninaamini yote tuliyoyajadili pamoja na michango yote ya Waheshimiwa Wabunge, ni kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Serikali, ambayo iliwasilishwa tukaijadili na kuipitisha hapa Bungeni ni ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Nne, baada ya uchaguzi wa Rais na Wabunge, uliofanyika mwezi Desemba, 2005. Bajeti hii imelenga kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua shilingi trilioni mbili, bilioni mia nne sitini mia tisa tisini na tano milioni; (shilingi 2,460,995 milioni), sawa na asilimia 14.5 ya Pato la Taifa. Serikali inaamini kwamba, lengo hilo litafikiwa. Hii inazingatia mwenendo mzuri wa ukusanyaji mapato ya ndani ya Serikali, unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania, ambapo kwa mwaka 2005/2006, wameweza kufikia kiwango cha juu cha ukusanyaji mapato cha shilingi bilioni 225.6 kwa mwezi Juni, 2006. Nachukua fursa hii kuupongeza uongozi na wafanyakazi wa *TRA* kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya. Aidha, nawataka sasa waongeze juhudi ili wakusanye mapato zaidi ya kiwango hicho kilichofikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha ukusanyaji wa mapato, kwa kupanua wigo wa kodi na kusimamia kwa karibu, mageuzi makubwa yanayoendelea ndani ya Mamlaka ya Mapato, chini ya mpango wake wa pili wa maboresho wa miaka mitano, ambao umekuwa msingi wa kukua kwa mapato ya ndani mwaka hadi mwaka. Aidha, tutaweka nguvu zaidi katika kuboresha usimamizi na utendaji wa Forodha, kwa kuongeza uwajibikaji, matumizi ya teknolojia ya kisasa na kupunguza kero za walipa kodi. Napenda niwakumbushe viongozi wote kwamba, wanawajibika kusimamia mikakati yote iliyowekwa katika kukusanya mapato na kusimamia matumizi ipasavyo.

Kwa upande wa Serikali za Mitaa, nasisitiza kwamba, ni wajibu wa Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa, na Majiji, kuhakikisha wanasaidia Mabaraza ya Halmashauri zao katika kuhimiza ukusanyaji mapato na kuoanisha mipango ya maendeleo na bajeti iliyopitishwa. Maeneo yaliyoonesha udhaifu na hasa yale yanayoainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali yaimarishwe.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyopewa kipaumbele katika bajeti ya mwaka 2006/2007 ni yale yaliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya

mwaka 2005 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA). Maeneo hayo ni pamoja na Kilimo, Elimu, Afya, Maji, Miundombinu, Nishati na Ardhi. Aidha, mgao wa fedha, umezingatia kuimarisha shughuli za Mahakama na masuala ya usalama wa raia. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa bajeti hii kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tukumbuke kwamba, maisha hayo bora tunayotaka kila mwananchi awe nayo, hayawezi kumfikia mwananchi bila utekelezaji wa mipango yetu kwa ukamilifu, hususan kupitia bajeti hii. Sote hapa tunawajibika kutekeleza yale tuliyoahidi. Waheshimiwa Wabunge, mnao wajibu mkubwa wa kufuatilia kwa karibu sana, yale yote tuliyokubaliana hapa. Serikali nayo kwa upande wake, itajitahidi kutekeleza ahadi zilizotolewa. Lengo ni kwamba, mwaka hadi mwaka, tuweze kupata matokeo halisi ya bajeti tunazozipitisha hapa Bungeni. Lazima tujione kwamba, kama viongozi, tunao wajibu wa kuwaletea wananchi maendeleo. Frantz Fanon**,** Mwandishi na Mwanafalsafa mahiri aliwahi kusema: "Kila kizazi kinao wajibu wa kutimiza ama unachagua kutimiza au kutupilia mbali."

Tunao wajibu wa kutekeleza. Tutimize wajibu wetu kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu. Serikali zilizotangulia, zimefanya kile walichoweza kufanya. Hatuna nafasi ya kuchagua kutotimiza wajibu wetu. Ni lazima tuutimize, sisi kama Wabunge ni lazima tusaidiane kuhimiza maendeleo sehemu zetu ili kumsaidia Mtanzania popote kupata maisha bora. Narudia, hatuna uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii ambayo tumeipitisha hapa Bungeni, ndiyo itakayotoa alama za ufanisi wetu katika mwaka wa kwanza wa kuiongoza nchi katika ngazi ya Vijiji, Majimbo, Wilaya, Mikoa na Taifa. Sisi Wabunge tuliopo ndani ya Bunge lako Tukufu, tuna wajibu wa kufanya kazi ya kusimamia yale tuliyokubaliana. Vigezo vya kumfanya mwananchi atupigie tena kura, vinaanza kutumika katika mwaka wa kwanza wa utumishi wetu na katika utekelezaji wa majukumu tuliyokabidhiwa. Katika hali hii, tunapimwa kwa uwezo na ufanisi wetu katika kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa. Mwandishi mmoja Henry Wadsworth Longfellow, alisema: "*We judge ourselves by what we feel capable of doing; others judge what we have done.*"

Tunajipima wenyewe kwa yale tunayodhani tunaweza kuyafanya, wengine watatupima kwa yale tuliyofanya. Tufanye yale tunayoweza kuyatekeleza kwa nguvu zote na tuanze kujipima wenyewe uwezo tulionao katika kutekeleza majukumu yetu tuliyokabidhiwa. Wananchi waliotuchagua, nao wanayo nafasi ya kutupima baada ya miaka mitano ijayo. Tukianza mapema kubainisha yale tunayopaswa kuyatekeleza na kuanza utekelezaji, sasa tutapata nafasi nzuri ya kupimwa na waliotupa madaraka ya kuongoza nchi hii.

Mheshimiwa Spika, viongozi ndio wanaoweza kutoa msukumo katika kuinua kipato cha wananchi. Uongozi una maeneo mengi, lakini moja na la muhimu ni sifa zinazomuwezesha kiongozi, kukubalika kwa anaowaongoza. Aidha, uwezo wa kufikiri, uwezo wa kujieleza, uwezo wa kuimudu kazi yake na kuelewa matokeo ya maamuzi anayoyafanya na jinsi yatakavyopokelewa na wanaoongozwa. Kuwa kiongozi mzuri,

inasaidia kuwa mtawala mzuri pia. Mwandishi mmoja Robin Sharma, aliandika kuhusu alichosema Woodrow Wilson kuhusu viongozi, nanukuu: *"You are not here to merely make a living. You are here in order to enable the world to live more amply, with great vision, with a finer spirit of hope and achievement. You are here to enrich the world, and you impoverish yourself if you forget the errand."*

Uongozi si lelemama, kiongozi yupo pale kuwawezesha wale anaowaongoza ili hatimaye waweze kufikia ndoto na matarajio yao. Kiongozi lazima aoneshe njia ya kufikia matarajio ya wale anaowaongoza. Kiongozi asiyeweza hali hiyo, atafutiwe jina lingine, si kiongozi pengine ni mfano wa kiongozi tu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa kazi nyingi za Serikali, unafanyika katika ngazi ya Halmashauri. Nililiarifu Bunge lako Tukufu mapema wakati nawasilisha Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwamba, Serikali Kuu itafanya Mkataba wa Kiutendaji na Halmashauri zote nchini ili kuweza kupima malengo tunayokubaliana. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kazi hiyo imeanza na mikataba imeandaliwa tayari kwa kuzishirikisha Halmashauri zote nchini na kwamba, hivi karibuni tutatia saini mikataba hiyo. Nasisitiza kwamba, utaratibu huu lengo lake ni kuongeza ufanisi, tija na kumuwezesha kila mmoja, kupimwa na kujipima mwenyewe ili wale watakaokiuka mkataba ule, waweze kuchukuliwa hatua kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji ni lazima uende sawia na matumizi ya rasilimali zinazotolewa kwa uangalifu na kwa mujibu wa taratibu za Serikali. Suala hapa siyo tu kwa Halmashauri kupata Hati Safi ya Mkaguzi Mkuu, suala liwe fedha zilizotolewa zimefanyia kazi gani. Hatutaki kuwianisha mahesabu peke yake, bali tunataka pia tuone matokeo ya kuboreshwa kwa utoaji huduma kwa wananchi. Kama fedha zilitolewa kwa Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa barabara, tunataka tuone barabara yenye ubora uliokusudiwa kwenye mkataba, kama ni ujenzi wa shule, tuone madarasa, maabara, maktaba na nyumba za walimu zenye ubora, kulingana na thamani ya pesa iliyotolewa. Naruadia maelekezo yangu kwamba, Kamati ya Uchumi na Fedha katika Halmashauri, iwe pia Kamati ya Kuhakiki na Kukagua Miradi inayotekelezwa katika Halmashauri hiyo. Hatutaki kuona mahesabu ya fedha bila kazi zilizotendeka na kwa ubora unaokubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amefanya mabadiliko makubwa ya uongozi katika ngazi zote. Matarajio ni kuona kwamba, ufanisi katika utendaji kazi unaongezeka. Mmoja wa washauri wa Serikali yetu aliwahi kusema, tatizo kubwa la watumishi wa umma na baadhi ya viongozi hapa Tanzania ni hodari wa kueleza kwa nini mambo mapya hayawezekani, badala ya wao kujiuliza kwa nini yasiwezekane. Maendeleo yetu yatachelewa sana iwapo tutaendelea kuwa wepesi wa kutosheka na maelezo kwa nini mambo hayawezekani, badala ya kuuliza kwa nini yasiwezekane. Maendeleo yanaletwa na wabunifu, wanaothubutu. Nasi Tanzania tunahitaji ubunifu zaidi, tunahitaji moyo wa kujituma zaidi na tunahitaji ujasiri wa kuthubutu zaidi. Lakini vilevile tunahitaji viongozi na watendaji wanaosikia na kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mfano mmoja, kuelezea hoja yangu. Bwana mmoja alikutana na rafiki yake, aliyekuwa amefiwa na mjomba wake, lakini rafiki mwenyewe alikuwa hasikii vizuri. Yule bwana akamsabahi, kisha kama ilivyo desturi, akampa pole kwa msiba uliomfika. Unasemaje? Sikusikii vizuri. Akajibu yule rafiki aliyefiwa; nasema hivi, pole kwa msiba wa mjomba wako. Bwana wewe, ongeza sauti, mimi sikusikii vizuri. Ikabidi sasa yule bwana avute pumzi na kupaza sauti kwa kadiri ya uwezo wake. P-o-l-e kwa ku-m-zi-ka m-jo-mba wa-ko!!! Kumbe ningefanyaje naye alikwisha kufa?

Watanzania wanatutegemea tuwasikilize na tuwasaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mkutano huu, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, walizungumzia zoezi la kuhamishwa wafugaji kutoka katika Pori la Akiba Usangu, hususan eneo la Ihefu. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, niliteua Kamati Ndogo ya Naibu Mawaziri, ambayo imeshughulikia suala hilo. Naibu Mawaziri hao ni Mheshimiwa Rita L. Mlaki, Naibu Waziri, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, Naibu Waziri, Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Naibu Waziri, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Celina O. Kombani, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed, Naibu Waziri, Wizara ya Usalama wa Raia. Naibu Mawaziri hawa walitembelea maeneo yanayohusika na kukutana na wananchi na viongozi na vilevile kujionea wenyewe hali halisi ilivyo. Kamati imewasilisha taarifa yao kwangu, kwa muda waliopewa. Napenda kutumia fursa hii, kuwapongeza kwa dhati Naibu Mawaziri hawa, kwa kuifanya kazi hiyo kwa umakini, umahiri na uharaka unaolingana na uzito wa suala hili. Aidha, Mawaziri wa Wizara hizo, wamekutana na Kamati hiyo, kupitia mapendekezo yao na kuyaafiki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kasoro ndogo ndogo zilizojitokeza katika zoezi la kuwahamisha wafugaji na mifugo yao kutoka ndani ya Bonde la Usangu, Kamati imeridhika kuwa zoezi hilo lilifanywa kwa uangalifu mkubwa na limefanikiwa. Napenda kutumia nafasi hii, kumpongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na viongozi wenzake. Hali ya Bonde la Ihefu, imeanza kubadilika na kwamba, maji yanaongezeka, uoto wa asili umeanza kuonekana na hata wanyama na ndege wameanza kurejea. Kamati imetoa mapendekezo yafuatayo ambayo Serikali katika ngazi mbalimbali itayafanyia kazi:-

- Hatua za dharura na za dhati zichukuliwe na viongozi wa Mikoa na Wilaya za kuwatengea wafugaji maeneo yao ya kufugia hasa wale walio katika maeneo ambayo uwezekano wa kuzuka migogoro kati ya wafugaji na wakulima ni mkubwa. Aidha, hatua hiyo ikamilike kabla ya mwezi Oktoba, 2006;

- Serikali ihakikishe kuwa maeneo wanayopelekwa wafugaji, yanapimwa na kujengewa miundombinu kama vile malambo na majosho. Aidha, Serikali itachukua hatua zitakazowezesha kupatikana kwa ruzuku ya dawa za mifugo ili kuwawezesha wafugaji kukabiliana na magonjwa ya mifugo;
- Uongozi wa Mkoa wa Mbeya uchukue hatua za dharura kutenga maeneo yaliyo mbali na vyanzo vya maji na hifadhi ya misitu kwa ajili ya mifugo iliyoko katika vijiji vya jirani na Ihefu wakati Serikali Kuu ikitafuta ufumbuzi wa kudumu kuhusu tatizo hili.

- Njia za kupitisha mifugo zifufuliwe;

- Kukamilisha Sera na Sheria itakayohakikisha kuwa wafugaji wanafuga kisasa na kibiashara;

- Kuwahamisha wafugaji katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya ufugaji na yasiyo na idadi kubwa ya mifugo na kuwapatia hati miliki kwa maeneo watakayopewa;

- Masoko ya nyama na viwanda vya kusindika nyama viongezwe ili kuwezesha uvunaji wa ng'ombe;

- Elimu itolewe kwa wafugaji juu ya athari za kuwa na mifugo mingi na faida ya kuwa na idadi ndogo ya mifugo yenye tija; na

- Kila Halmashauri ipange matumizi mazuri ya ardhi *(Land Use Masterplan)*, kwa sekta mbalimbali, kama vile makazi, mifugo, kilimo, viwanda, hifadhi, miundombinu, huduma za jamii na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Katiba na Sheria, Usalama wa Raia, Maendeleo ya Mifugo na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, kwa kushirikiana na uongozi wa mikoa na wilaya, wanalo jukumu sasa la kuandaa programu ya utekelezaji wa mapendekezo hayo ili tuwawezeshe wafugaji, kutulia na kuendeleza mifugo kwa manufaa yao na Taifa kwa ujumla. Aidha, tutakuwa na mkutano wa wadau wote wa mifugo tarehe 3 Oktoba, 2006 Mkoani Mbeya, kutathmini hatua zilizochukuliwa na hali ya baadae, ambapo mimi mwenyewe ndiye nitakayekuwa Mwenyekiti wa kikao hicho. Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, itaongoza kazi ya utekelezaji wa maamuzi haya yote ikiwa ni pamoja na kufanya maandalizi yote muhimu ya mkutano huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilimo bado ni mhimili wa uchumi wa Taifa letu. Kilimo bora na cha tija, kinahitaji matumizi bora ya pembejeo ikiwemo mbolea. Mahitaji ya mbolea kwa ujumla yameongezeka, japo matumizi yake hayajafikia kiwango cha kitaalam, kinachopendekezwa kwa kila hekta moja. Matumizi yameongezeka kutoka tani 112,000 mwaka 2004/2005 hadi tani 120,000 mwaka 2005/2006, ongezeko la asilimia saba. Pamoja na ongezeko hilo, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ametueleza hapa Bungeni kwamba, matumizi ya mbolea nchini ni wastani wa kilo nane za virutubisho kwa hekta kwa mwaka badala ya wastani wa kilo 60 kwa hekta kwa mwaka, kiwango ambacho ndicho kinachopendekezwa na wataalam. Nchi nyingine duniani, zinatumia viwango vikubwa zaidi. Kwa mfano, jirani zetu Malawi, wanatumia wastani wa kilo 27, Afrika Kusini kilo 63.

Mheshimiwa Spika, tumesikia hapa Bungeni baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wakilalamikia bei na upatikanaji wa pembejeo za kilimo. Aidha, mikoa mingi niliyofanya ziara na kuongea na wananchi, walilalamikia pia hali hii, hasa bei ya mbolea kuwa kubwa licha ya Serikali kutoa ruzuku na dawa ya *Sulphur* ya kutosha

kutopatikana kwa wakulima wa korosho. Kwanza, kwangu mimi malalamiko haya yametafsiriwa kwa lugha ya kimaendeleo. Hii ni hatua ya kupongeza. Ukisikia mwananchi anaulizia mbolea au dawa za kuulia wadudu waharibifu, basi huyu ni mwananchi anayetaka maendeleo. Tumeongeza ruzuku ya pembejeo kutoka shilingi bilioni saba hadi shilingi bilioni 21 mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kusaidia wakulima kupata pembejeo ikiwemo mbolea, mbegu bora na dawa ya *Sulphur*, kwa ajili ya mikorosho. Pengine fedha hizi haziwezi kushusha bei ya pembejeo kwa kiasi cha kumridhisha kila mmoja wetu. Lakini naamini zitatoa nafuu kubwa. Uongozi wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na ule wa Mikoa, lazima usimamie zoezi hili ili mkulima afikishiwe pembejeo kwa wakati na kwa bei nafuu. Tunasema ni lazima kilimo kiwe ni kazi ya kufa na kupona. Tukiamua na kudhamiria kukiimarisha kilimo chetu, tunaweza kufanikiwa tena kwa ubora zaidi. Tunaweza na sote tuseme hivyo na tukasimamie maendeleo ya sekta hii muhimu kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya nchi yetu yanategemea vilevile jinsi tunavyojizatiti, kuimarisha elimu nchini. Wakati wa ziara yake Mkoani Mara, wiki iliyopita, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alitutahadharisha kujiandaa kupokea katika shule za sekondari, watoto wengi watakaomaliza darasa la saba mwaka huu. Katika mwaka wa 2005, jumla ya wanafunzi 493,946 wa darasa la VII walifanya mtihani. Katika mwaka huu wa 2006, wanafunzi 679,050 wamejiandikisha kufanya mtihani wa darasa la VII. Tukitarajia kuwa asilimia 70 ya wanafunzi hao, watafaulu mtihani huo, idadi ya watakaofaulu itakuwa 475,335. Aidha, kwa kutarajia kuwa asilimia 60 ya hao watakaofaulu wataingia sekondari, tunahitaji nafasi za kutosheleza watoto 285,201 katika sekondari nchini. Hii ni changamoto kubwa sana kwetu sote. Kila mkoa utahitaji kuongeza vyumba vya madarasa ili wanafunzi wote hawa, wapate nafasi ya sekondari. Takwimu zilizopo zinaonesha kuwa, mikoa itakayohitaji kuongeza vyumba vya madarasa zaidi ni pamoja na Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Morogoro, Dodoma, Dar es Salaam, Kigoma, Mbeya na Mtwara, wale wengine wanahitaji lakini hawa wanahitaji zaidi. Nawaelekeza Wakuu wa Mikoa, kuongeza juhudi za kukabiliana na hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, barabara zina mchango mkubwa sana katika kufanikisha vita dhidi ya umaskini na pia kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005. Miundombinu ni sawa na moyo kwenye mwili wa binadamu na barabara ndiyo mishipa yake. Katika uchumi barabara na reli ndizo muhimu zaidi katika kuongeza kipato cha wanyonge walio wengi na pia katika kupambana na umaskini. Wingi na ubora wa miundombinu ni sharti la kwanza kabisa katika kuchochea ongezeko la uzalishaji wa mazao na bidhaa za viwandani na hivyo kukuza uchumi wa kaya na Taifa kwa ujumla. Kwa hiyo, mtandao mpana na bora wa barabara hadi vijijini, unachochea uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na pia unasaidia wananchi kufikiwa na huduma kama vile za kibenki, umeme, simu, elimu na afya na hivyo, kurahisisha ushiriki wa wananchi katika shughuli nyingine za kijamii. Kwa maana hiyo, barabara ni kiungo muhimu katika kutekeleza lengo la maisha bora kwa wote.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu, tatizo la kukosekana mtandao mzuri wa barabara nyingi na bora hadi maeneo ya vijijini, bado ni kubwa. Baba wa Taifa,

Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliwahi kusema: *"People have gone to the moon and we are still trying to reach the village and the village is getting further away."*

Kwa Kiswahili ni kwamba, watu wengine wamefika kwenye mwezi, sisi bado tunahangaika kutaka kufika kijijini ambapo kijiji chenyewe kinazidi kuwa mbali. Hii ndiyo hali tunayopambana nayo na *Inshallah* tutafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mtandao wa barabara za lami nchini, umekuwa ukitekelezwa kwa kiasi kikubwa sana kwa kutumia mikopo kutoka taasisi za fedha za kimataifa na kutoka kwa wafadhili. Hata hivyo, kuanzia mwaka 2001, ambapo hali ya kiuchumi nchini ilianza kuimarika zaidi, Serikali iliamua kuanza kutenga angalau shilingi bilioni 1.84 kila mwezi ili kutekeleza miradi ya barabara kuu za lami, ambayo kwa vigezo vyetu ni muhimu hata kama wahisani na taasisi za fedha za kimataifa zinazotoa mikopo hazikuafiki. Katika miaka mitano hiyo, miradi kadhaa mikubwa ya barabara na madaraja katika Kanda za Ziwa, Kati na Kusini, yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 500 imejengwa au kuendelea kujengwa kwa kutumia bajeti yetu ya ndani pekee. Hivi sasa tunaendelea kutekeleza miradi ya barabara yenye jumla ya kilometa zipatazo 754, kwa gharama ya karibu shilingi bilioni 320. Kati ya hizo tayari kilometa 162 za lami zimekamilika na kazi zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, barabara zinazohitaji kujengwa kwa kiwango cha lami bado ni nyingi kuliko fedha zilizopo. Uamuzi wa wapi tuanze kujenga barabara zipi, uko kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na hutegemea upatikanaji wa fedha. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, inaelekeza kuanza kwa kukamilisha miradi iliyokwishaanza, halafu zile barabara zinazounganisha nchi yetu na nchi jirani na zinazounganisha mikoa yetu. Kwa mfano, ukiacha miradi inayoendelea ukanda wa Kusini na Kati, maandalizi ya utekelezaji wa barabara ya Masasi - Tunduru - Songea - *Mbamba Bay,* Tunduma - Sumbawanga - Mpanda - Kigoma, Musoma - Mugumu - Loliondo - Mto wa Mbu na ujenzi wa daraja katika Mto Malagarasi ni ushahidi wa kipaumbele ambacho Serikali imeanza kuweka katika kuboresha miundombinu ya barabara katika maeneo makubwa yenye umuhimu mkubwa kiuchumi na kijamii nchini. Aidha, ukiacha barabara hizi kuu, Mheshimiwa Rais amesisitiza umuhimu wa kuweka mkazo katika Barabara za Mikoa ili zipitike wakati wote. Serikali itazingatia vipaumbele hivyo na maelekezo ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, katika mijadala iliyoendelea humu Bungeni, usafiri wa wanafunzi katika Jiji la Dar es Salaam ulijadiliwa sana. Suala la usafiri wa wanafunzi Dar es Salaam ni kero kubwa kwa wazazi, wanafunzi na viongozi wa jiji na hata wenye vyombo vya usafiri. Hivi sasa inakadiriwa kwamba, wapo wanafunzi zaidi ya 150,000, ambao wanahitaji usafiri kila siku Jijini Dar es Salaam. Aidha, inakadiriwa kuwa, kuna daladala takriban 6,000, zikiwemo daladala ndogo 5,000 Jijini Dar es Salaam. Uzoefu unaonesha kwamba, daladala ndogo zinazotakiwa kubeba abiria kati ya 13 – 15, akiwemo dreva na kondakta, sasa zinabeba ujazo wa abiria kati ya 15 - 18. Aidha, yapo magari mengine madogo, ambayo yanabeba abiria kati ya 22 - 26. Pamoja na uwezo halisi wa magari hayo, ni ukweli vilevile kuwa, magari madogo mengi yameongeza viti vya kubeba abiria zaidi kati ya wanne hadi nane. Pamoja na hali hii ya kuongeza nafasi za

abiria, ambazo haziko katika utaratibu wa Sheria za Usalama Barabarani, bado tatizo la wanafunzi ni kero kubwa na halijaweza kutatuliwa. Serikali inatambua tatizo hili ambalo linagusa sana jamii, hususan wananchi wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi katika Jiji la Dar es Salaam na Miji mingine mikubwa kama Mwanza, Arusha na Tanga, kwa sehemu kubwa hutumia magari ya usafiri yanayomilikiwa na watu binafsi, ambayo huendeshwa kibiashara. Wanafunzi hutozwa nauli ya shilingi 50/= kwa Jiji la Dar es Salaam. Kutokana na nauli kuwa ndogo, madreva wa vyombo vya usafiri, huwaacha wanafunzi katika vituo vya usafiri. Aidha, baadhi ya wazazi, hupenda kuwapeleka watoto wao katika shule zilizoko mbali na wanakoishi, kwa kudai kuwa shule hizo ni bora zaidi. Tatizo hili la usafiri Jijini Dar es Salaam, linaathiri ubora wa elimu, kwa kuwa linasababisha kuchelewa, uchovu na utoro wa wanafunzi. Vilevile linasababisha bughudha, kunyanyasika na hivyo, kuathiri wanafunzi kisaikolojia. Ili kulitafutia ufumbuzi suala hili, nimewataka Mawaziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na Waziri wa Miundombinu, kuchukua hatua kadhaa zikiwa ni pamoja na zifuatazo:-

- Kufanya utafiti ili kubaini mahitaji halisi ya shule, vyumba vya madarasa na walimu katika maeneo yote ya Jiji;

- Kuhamisha wanafunzi kwenda shule za msingi zilizo jirani na maeneo wanakoishi baada ya kufanyika utafiti;

- Kuandikisha wanafunzi wa darasa la kwanza katika mitaa wanamoishi kwa kuzingatia Waraka wa Elimu Na. 4 wa mwaka 2005;

- Kufanya mazungumzo na wamiliki wa vyombo vya usafiri kwa mfano, Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA), ili kuona namna ambavyo vyombo hivyo vinaweza kushirikiana na Serikali katika kutatua tatizo hili kwa wale wanafunzi wachache watakaokosa nafasi maeneo wanakoishi;

- Kuendelea kushirikisha wadau mbalimbali kama vile Usalama wa Raia, *SUMATRA*, Chama cha Wenye Mabasi ya Daladala Dar es Salaam na wengine katika kusimamia huduma ya usafiri kwa wanafunzi;

- Kutoa elimu kwa wazazi na jamii ili wapokee na kushiriki kwenye utekelezaji wa mikakati hii.

Mheshimiwa Spika**,** pamoja na hatua hizo, Serikali kwa kushirikiana na wadau wanaohusika, itabidi itekeleze mikakati ya muda mrefu ifuatayo:-

- Kwa kutumia matokeo ya utafiti *(School Mapping* na *Micro-planning)*, kujenga shule mpya kwenye maeneo stahili, kuongeza vyumba vya madarasa na kuwapanga walimu kwa uwiano mzuri zaidi;

- Kuihusisha na kuishawishi sekta binafsi kuwekeza katika vyombo vya usafiri wa wanafunzi; na

- Pengine Viongozi na Watendaji wa Mkoa wa Dar es Salaam, itabidi wachukue hatua za kujifunza kutoka nchi zilizofanikiwa kutatua tatizo la aina hiyo kule Ethiopia, Addis Ababa.

Mheshimiwa Spika, yapo malalamiko kutoka kwa wananchi kwamba, licha ya kuondoa kodi kwa baadhi ya bidhaa muhimu kama vile mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa, bado bei za bidhaa hizo hazijashuka, kutoa unafuu uliotarajiwa na wananchi wengi. Hili ni tatizo ambalo ni kero kwa wananchi. Hata hivyo, utafiti unaonesha kwamba, bei zinapopunguzwa na Serikali, wapo wafanyabiashara wanaotumia nafasi hiyo, kwa kuchelewesha matumizi ya bei mpya kwa kisingizio kwamba, bado wanayo mafuta ya akiba ya zamani hivyo, wanaendelea kuyauza kwa bei ya juu. Lakini ni wafanyabiashara hao hao, ambao kama bei ikipandishwa, nao wanapandisha mara moja, bila kujali kama walikuwa na akiba ya zamani ya mafuta, ambayo waliinunua kwa bei ya chini. *(Makofi)*

Kwa vyovyote vile, huu siyo uungwana katika biashara. Huu ni ubinafsi wa kutaka kujipatia faida ya haraka haraka, bila kuwajali wadau wa bidhaa hii ya mafuta. Napenda kuchukua nafasi hii, kuvitaka vyombo vinavyoshughulikia suala la mafuta, vifuatilie kwa karibu na kuhakikisha kuwa, maamuzi ya Serikali ya kuleta unafuu wa bei za mafuta unawanufaisha wananchi. Aidha, napenda kurejea uamuzi wa Serikali wa kuiruhusu *TPDC*, kuingia katika uagizaji mafuta nchini. Lengo letu ni kuleta changamoto katika ushindani wa biashara ya mafuta. Tumeiruhusu pia *TPDC*, kuanzisha utaratibu wa kuweka akiba ya mafuta ili pale panapotokea matatizo, nchi yetu iweze kukabiliana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika**,** suala la mafao ya mirathi kwa wanawake wajane na pensheni kwa wastaafu, ambao hawakuingizwa katika Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Umma, bado ni tatizo kubwa. Waheshimiwa Wabunge, mmelizungumzia suala hili kwenye Mkutano huu, kwa uchungu mkubwa sana. Wajane na wastaafu hao, wanapata usumbufu kwa kucheleweshewa mafao hayo. Hili ni tatizo ambalo ni kero kwa wajane na wastaafu, kwa kipindi cha muda mrefu sasa. Zipo taarifa kuwa, hata pale nyaraka zinapokuwa zimekamilika, bado upo ucheleweshaji usio wa lazima katika taasisi za Serikali zinazoshughulikia suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika**,** ucheleweshaji wa malipo ya mirathi, huchangiwa vilevile kwa kiasi kikubwa na wategemezi kutofahamu taratibu zinazopaswa kufuatwa ili kuwezesha kulipwa kwa malipo ya mirathi. Wizara ya Fedha itapaswa kuchukua hatua zifuatazo:-

- Kuwaelimisha wananchi kwa ujumla, taratibu wanazopaswa kufuata wakati wa kuwasilisha na kufungua mirathi ili kuondoa tatizo hilo;

- Kuwaelimisha wananchi kuhusu kuhusika kwao katika kuchelewesha malipo ya mirathi, hasa pale kunapotokea kutokubaliana kwa wanandugu katika uteuzi wa Msimamizi wa Mirathi;

- Kwa vile Mahakama ndizo ambazo zinahusika katika kufungua mirathi, kuwathibitisha wasimamizi wa mirathi, kutoa viapo kwa Wasimamizi wa Mirathi na hatimaye kufanya malipo, itabidi Mahakama nayo ishirikishwe kikamilifu;

- Kushirikiana na waajiri kuondoa tatizo la ucheleweshaji wa malipo ya mirathi, kwa kuboresha mawasiliano kati ya waajiri na wasimamizi wa mirathi, pamoja na Hazina kuhusu mapungufu yoyote yanayoathiri ulipaji wa malipo ya mirathi mara yanapojitokeza;

- Kuwaelimisha wategemezi kuzitumia Ofisi za Hazina Ndogo, ambazo zipo katika kila Mkoa katika kuwasilisha hoja zao mbalimbali badala ya kusafiri hadi Hazina Makao Makuu, Dar es Salaam kufuatilia malipo yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutoa elimu, Wizara ya Fedha itachukua hatua zifuatazo:-

- Kuwahamishia sehemu kubwa ya Wastaafu katika Mifuko ya Pensheni ya *GEPF*, *SPF* na *PPF;*
- Kuanzisha Idara mpya ya Pensheni ambayo itaendelea kuwahudumia wastaafu ambao watakuwa hawajahamishiwa kwenye mifuko hiyo;

- Kuteua watendaji ambao watapewa jukumu maalum la kufuatilia na kuona kuwa hoja mbalimbali zinazoibuliwa na wakaguzi zinajibiwa kwa wakati na wote wanaohusika;

- Kuimarisha mawasiliano kati ya Ofisi za Hazina Ndogo na Wizara husika ili kupunguza urasimu usio wa lazima na bila kukiuka kanuni na taratibu za fedha.

- Katika muda wa miezi sita, Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Ofisi zote za Hazina Ndogo, iwe imetayarisha orodha ya wajane wote, ambao malipo ya mirathi yao imechukua muda mrefu na ibainishe kasoro zilizosababisha ucheleweshaji huo na ichukue hatua kuwasaidia kuzirekebisha kwa kushirikiana na waajiri. Nitapenda kupata taarifa hiyo mara baada ya kazi hiyo. Kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane kupambana na tatizo hili, kwa kuwasaidia hao wanaopata matatizo. *(Makofi)*

Kwa upande wa waajiri, ninawataka kila Wizara, Idara inayojitegemea na Wakala wa Serikali, wahakikishe kuwa wapo watumishi katika Idara ya Utawala na Utumishi, ambao wanapewa jukumu maalum la kufuatilia wao wenyewe, masuala ya watumishi wao waliostaafu na kuwaarifu ipasavyo kila mara hadi malipo yao yanapopatikana.

Kwa vile suala la mirathi linahusisha vilevile Mahakama, natoa wito maalum kwa Mahakama zetu, kulipa suala la mirathi uzito unaostahili ili mashauri ya aina hiyo, yachukue muda mfupi kadri inavyowezekana. Ni matumaini yangu kwamba, tukiweka ushirikiano kwa kuwaelimisha wananchi, tatizo hili litakamilika kwa mafanikio na hivyo kumaliza kero hii ambayo imedumu kwa muda mrefu nchini.

Mheshimiwa Spika, dhana ya ujasiriamali inamhusu mtu mmoja mmoja au vikundi vinavyoungana pamoja ili kutekeleza shughuli za uzalishaji mali. Sote tumekuwa tukisikia maelezo kuwa, Watanzania bado tupo nyuma katika shughuli za biashara na uwekezaji ukitufananisha na wenzetu wa nchi zinazotuzunguka. Serikali imeweka sera na mazingira mazuri, yanayowezesha wananchi kutekeleza kazi mbalimbali zinazowaongezea kipato. Kwa hiyo, Serikali imeweka fursa, imetunga sera na sheria mbalimbali za kuwawezesha wananchi kunufaika; imeanzisha mifuko yake, lakini vilevile imewezesha Benki za Biashara kuwekeza na hivyo kuwapa wigo wa utoaji wa mikopo midogo midogo kwa wajasiriamali. Wachina wana methali isemayo **“**Niambie nami nitasahau, nioneshe nami ninaweza kukumbuka, lakini nihusishe nami nitaelewa zaidi.” *(Makofi)*

Serikali inachukua hatua za kujenga Jeshi imara la wajasiriamali. Lengo letu ni kuwawezesha wananchi watambue kuwa hatua zozote zinazochukuliwa na Serikali, zinatakiwa ziwawezeshe kuthubutu kuanzisha miradi endelevu; kuwekeza na hata kujiunga katika Vyama vya Ushirika na *SACCOS*, ili kuwawezesha kuweka nguvu zao pamoja, kwani kama tunavyoelewa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Kwa Watanzania wenzangu, napenda nisisitize kuwa, kuongezeka kwa ukuaji wa uchumi katika ngazi zote, kunatutegemea sisi wenyewe kila mmoja wetu kwa nafasi yake. Mustakabali wa maisha yetu, upo mikononi mwetu sisi wenyewe. Tusipende kujirudisha nyuma, tuanze kuchangamka. Wakati wa Maonesho ya Saba Saba, tumeona juhudi za vikundi vya wanawake nchini za kujiongezea kipato, kwa mfano, mama lishe na viwanda vidogo vya kusindika mazao. Watu hawa wangepata mikopo, wangeenda kwa kasi kubwa zaidi. Kwa hiyo, natoa wito kwa wajasiriamali wote nchini, kutumia mikopo midogo midogo, kupanua shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa upande wake, itaendelea kuchukua hatua kuwajengea wananchi uwezo kiuchumi. Kama Bunge hili lilivyoelezwa katika Mkutano huu wa Nne, Serikali imetenga wastani wa shilingi milioni 500 kwa kila Mkoa kwa mwaka 2006/2007, kama mbegu ya kuwawezesha wajasiriamali nchini, kupata mitaji midogo midogo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kutokana na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na matumaini makubwa yaliyojengwa kwa wananchi kutokana na uamuzi huo, Mheshimiwa Rais, ameamua kuongeza fedha za Mfuko huo ili sasa kila Mkoa uweze kupata zaidi ya wastani wa shilingi bilioni moja. Ili kukuza uelewano miongoni mwa wadau mbalimbali, utakaoleta ufanisi wa utekelezaji wa ahadi hii, napenda kusisitiza mambo yafuatayo juu ya dhamira hii ya Serikali kuhusu mpango huu:- *(Makofi)*

- Serikali itatoa jumla ya shilingi bilioni 21 chini ya mpango huu, ambazo zitapitia kwenye mikondo miwili itakayohusisha taasisi za fedha na benki mbalimbali zilizopo nchini.

- Mkondo wa kwanza ni kupitia kundi la mabenki kama *CRDB* na *NMB*, ambayo yako tayari kutoa mikopo ya aina hiyo, kwa kutumia fedha zao, kwa kupewa dhamana na Serikali, lakini kwa riba ya asilimia kumi kwa mwaka. *(Makofi)*

- Mkondo wa pili, ni kukopesha moja kwa moja kupitia benki zenye mitaji midogo na taasisi nyingine za fedha kama vile Benki ya Posta; Benki za Wananchi kama vile *Mufindi Bank, Mbinga Bank, Mwanga Bank, Dar es Salaam Community Bank; EXIM Bank*, Benki ya Akiba; *SCCULT,* Mifuko ya Maendeleo ya Wanawake na Vijana na Asasi nyingine za fedha ambazo hivi sasa zinatoa huduma za mikopo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekubali kutumia mifumo ya makundi hayo mawili ya mabenki. Serikali imefikia uamuzi huo, kwa vile asasi hizo zikihusika kwa wakati mmoja katika kutekeleza uamuzi huu, mikopo mingi itatolewa na kwa wajasiriamali wengi na kwamba, utaratibu huu utatuwezesha kupata mafanikio yaliyokusudiwa katika kipindi kifupi. Kwa mfano, kwa kupitia kundi la kwanza, la Benki za *CRDB* na *NMB* utawezesha kupanua uwezo wa kukopesha kwa mara tatu au zaidi ya kiwango cha dhamana itakayowekwa na Serikali. Serikali ikiweka akiba kwenye Mfuko huo wa shilingi bilioni 10.5, uwezo wa kukopesha utapanuka hadi shilingi bilioni 31.5 au zaidi. Fedha za mikopo kutoka kwenye mikondo hii miwili ya asasi za fedha zitatolewa kwa *SACCOS*, vikundi ambavyo vina shughuli za uzalishaji mali au za kibiashara na wajasiriamali mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaunda Kamati ya Wataalam chini ya Uenyekiti wa Benki Kuu ya Tanzania, ambayo itakuwa na jukumu la kuidhinisha malipo kwa benki hizo, pale ambapo mkopaji ameshindwa kurejesha mkopo unaohusika. Hata hivyo, ieleweke kuwa, wakopaji watachukuliwa hatua za kisheria kulingana na mikataba watakayowekeana na vyombo vya fedha chini ya utaratibu huu. Fedha hizi lazima zirejeshwe, fedha hizi si sadaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kufafanua mambo mengine machache kuhusu taratibu na kanuni za mpango huu.

Kwanza, kiwango halisi cha fedha zitakazotolewa kwa kila Mkoa, kitatofautiana baina ya Mkoa na Mkoa kuzingatia vigezo maalum vitakavyopangwa, kama vile wingi wa idadi ya watu. Kwa hiyo, licha ya zile shilingi bilioni moja Kimkoa, zile nyingine zitategemea idadi ya watu na kadri watakavyoomba.

Pili, fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya wajasiriamali wa Vijijini na Mijini, hususan walioko kwenye *SACCOS,* Ushirika, vikundi vya uzalishaji mali na wajasiriamali mmoja mmoja.

Tatu, fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya mikopo yenye masharti nafuu. Kiwango cha riba cha awali kilichokubalika ni asilimia kumi kwa mwaka.

Nne, Serikali inatambua kuwa, vyombo vya fedha vitakavyoshiriki katika utoaji mikopo hii, bado havijaenea katika Mikoa/Wilaya zote nchini na uwezo unatofautiana kama alivyotuambia Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo jana. Hivyo, kila Mkoa/Wilaya itapewa fursa ya kubainisha ni vyombo vipi vinaweza kutekeleza jukumu hili kwa ufanisi katika maeneo yao. *(Makofi)*

Tano, msukumo utakuwa ni mikopo hii kutolewa na mabenki husika kupitia *SACCOS*. Pale ambapo *SACCOS* hazipo, viongozi na hasa Waheshimiwa Wabunge, wahusike katika kuhamasisha wananchi kuzianzisha. Lakini nasisitiza kwamba, tahadhari ichukuliwe katika uanzishaji huo, tusije kuanzisha *SACCOS,* ambazo sio mahiri, zitakazolenga kuchukua mikopo hii tu na kisha kutoweka.

Sita, utaratibu wa kutoa mikopo utaweka kipaumbele katika miradi ya uzalishaji mali kwa mfano, kilimo, ufugaji, uvuvi, viwanda vidogo vidogo, ufugaji nyuki na kadhalika, sio kwenye biashara pekee, tusije tukajenga Taifa la wachuuzi. Aidha, *SACCOS* na vikundi vya ufundi na vya viwanda vidogo vidogo *(SIDO)*, vinahimizwa kutoa mikopo hii kwa njia ya kutoa zana au pembejeo, kulingana na mazingira yake na makubaliano na mkopaji. *(Makofi)*

Saba, Serikali inakusudia kuweka mfumo thabiti wa usimamizi na uratibu katika ngazi ya Kitaifa, Mkoa, Wilaya na kwenye Kata, kwa kutumia vyombo mbalimbali vilivyopo. Azma hii itapunguza gharama za utoaji mikopo kwa walengwa na inasisitizwa kuwa, hakutakuwa na kugawana posho kwa wajumbe wa vikao husika katika ngazi zote. Fedha hizi sio za kugawana posho. Katika ngazi ya Taifa, Serikali itaunda kamati ndogo ya ushauri itakayowahusisha baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, ambayo jukumu lake litakuwa ni kuishauri Kamati ya Kitaifa ya Uwekezaji ya Baraza la Mawaziri, itakayohusika na usimamizi wa mpango huu. Katika ngazi ya Mkoa, kutakuwa na Kamati ya Uratibu na Ufuatiliaji itakayojumuisha wataalam wachache wa fani mbalimbali ndani ya Sekretarieti ya Mkoa na Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya, chini ya Uenyekiti wa Mkuu wa Mkoa.

Nane, ili kuimarisha umiliki wa mpango huu, Kamati ya Fedha na Uchumi ya kila Halmashauri, itahusishwa kupitia na kupitisha maombi ya miradi iliyoibuliwa na wajasiriamali wa Wilaya zao. Serikali inatarajia kuwa, hakutakuwepo urasimu kwenye Halmashauri kupitisha miradi ya walengwa. Kamati za Uwezeshaji za kila Kata, zinahimizwa kuhamasisha wajasiriamali na kuratibu mpango huu katika ngazi hiyo.

Tisa, Serikali na vyombo vya fedha husika, tumebaini kuwa kuna upungufu mkubwa wa wataalam wa kutoa na kusimamia mikopo katika mabenki na asasi nyingine za fedha.

Kwa hiyo, Benki Kuu na asasi za kifedha, vitatoa mafunzo ya haraka ya wataalam wa ziada kwa vyombo vya benki vitakavyohusika ili kuondoa tatizo la upungufu wa

wataalam wenye uwezo kusimamia mikopo. Mafunzo hayo yatajumuisha vilevile Maafisa wa Wilaya wafuatao kutoka kwenye Wilaya; Maafisa Ushirika, Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Mipango. *(Makofi)*

Kumi, ili wajasiriamali wapewe uwezo wa kuandaa na kuwasilisha miradi inayokopesheka, Wizara husika chini ya Uenyekiti wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, zimepewa jukumu la kuandaa mpango maalum wa mafunzo ya wataalam, watakaosaidia uandaaji miradi ya wajasiriamali. Wakati mafunzo hayo yanaandaliwa, Benki Kuu na vyombo vingine vinavyohusika kutoa mikopo vitaweka utaratibu wa kutumia wataalam elekezi kusaidia wajasiriamali.

Kumi na moja, sambamba na hatua hizo, Serikali itashirikiana na wadau mbalimbali kutoa elimu ya umma kuhusu mpango huu.

Mheshimiwa Spika**,** ili kuwezesha wananchi wengi kunufaika na mpango huu, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, kuhamasisha wajasiriamali katika Halmashauri zao kuibua miradi mizuri yenye faida, itakayoweza kukidhi vigezo vya kibenki vya utoaji mikopo kupitia mpango huu.

Mheshimiwa Spika, uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa Programu mbalimbali, zinazolenga kutoa huduma za fedha Vijijini, zimeonesha kuwa, kuna fursa kubwa kwa wananchi wenye kipato kidogo Vijijini kufanya yafuatayo:-

- Kutambua umuhimu wa kuweka akiba na kukopa ili kuimarisha upatikanaji mitaji ya uwekezaji vijijini; azma hii imeanza kukuza na kujenga utamaduni wa kujiwekea akiba na kukopa, ndiyo maana ya hizo *SACCOS.*

- Kuhamasishana ili kujiunga pamoja na kuanzisha vikundi imara vya kuweka na kukopa *(SACCOS/SACCAS).*

- Kutambua umuhimu wa kutumia asasi za kifedha za vijijini kupata huduma za kifedha bila kusubiri mabenki na hivyo kujiletea maendeleo ya haraka, hususan katika kujiongezea kipato, kuongeza ajira na hatimaye kusukuma kwa kasi zaidi vita dhidi ya umaskini.

- Kujenga utamaduni na tabia ya kukopa na kurejesha mikopo kwa wakati hivyo, kuzifanya *SACCOS* kuwa vyombo vyenye sifa ya kukopesheka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uzoefu nilioueleza, kuanzishwa kwa *SACCOS* nyingi, kutapunguza tatizo la kupata huduma za fedha vijijini. *SACCOS* ni njia endelevu ya wananchi kujipatia mitaji kwa ajili ya uwekezaji vijijini. Aidha, *SACCOS* zinasaidia kukopesha wanachama wake kwa masharti nafuu na bila kuwa na dhamana rasmi. Vilevile, *SACCOS* ni mikondo mizuri ya kujenga kada imara ya wajasiriamali, ambao wako tayari kutumia fursa za mitaji zinazojitokeza kujiletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika**,** wakati nikiwasilisha hoja ya utaratibu huu wa mikopo, nilisema Wabunge watahusishwa kikamilifu. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ameteua wafuataao kuwa Wajumbe wa Bodi ya Ushauri; Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Mohammed G. Dewji, Mheshimiwa Adam K. A. Malima, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa. Martha J. Umbulla na watu wengine watatu ambao ni Ndugu Shamimana Ntuyabaliwe, Ndugu Grace Rubambe na Ndugu Marcelina Chijoriga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana wakati wa kujadili hoja ya Waziri wa Fedha, rafiki yetu mmoja wa Upinzani alidai kwamba, kwa uamuzi wa Mheshimiwa Rais, kuidhinisha nyongeza ya fedha hizi eti amevunja Katiba. Mheshimiwa Rais, hakuvunja kifungu chochote cha Katiba. Kama alivyoeleza Waziri wa Fedha, sehemu ya fedha hizi zitatoka kwenye Bajeti ya Serikali kwa mwaka huu wa fedha na nyingine kwenye Taasisi za Fedha, kwa maelewano maalum kati ya Serikali na taasisi hizo. Sasa Katiba imevunjwa wapi? *(Makofi)*

Pili, kwa hakika Mheshimiwa Rais wetu, sio amevunja Katiba, ametekeleza kikamilifu Katiba ya nchi yetu, maana Ibara ya 9(i) inasema ifuatavyo na mimi ninanukuu kwamba: “Matumizi ya utajiri wa Taifa, yanatilia mkazo maendeleo ya wananchi na hasa zaidi yanaelekezwa kwenye jitihada ya kuondosha umaskini, ujinga na maradhi.” *(Makofi)*

Lakini ninaelewa hisia za Wapinzani wetu. Jitihada hizi za Serikali zikisimamiwa vizuri zikafanikiwa, maisha bora yatapatikana kwa kila Mtanzania. Pengine hayawezi yakamletea faraja sana rafiki yangu, aliyesema hoja hiyo jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha, napenda nizungumzie suala muhimu linalohusu afya za Waheshimiwa Wabunge. Shughuli za Bunge, zinawahitaji Waheshimiwa Wabunge, kutumia muda wao mwingi wakiwa kwenye vikao. Ratiba ya Mikutano ya Bunge, Kamati za Kudumu za Bunge na semina za mwisho wa wiki inaonesha kuwa Waheshimiwa Wabunge wanatumia karibu siku 138 kwa mwaka katika vikao hivyo. Hii ni sawa na takriban miezi minne ya kukaa tu. Aidha, kwa siku hizo tunatumia karibu saa 940 za kukaa tu kwenye vikao. Kazi hii ya kukaa kwenye vikao, haihitaji nguvu nyingi na kwa hiyo, kalori zinazochomwa kwenye mwili ni chake sana. Katika zoezi la kupima afya za Waheshimiwa Wabunge, lililofanywa na Madaktari Bingwa walioongozwa na Profesa Lwakatare hivi karibuni, wataalam hao wanatueleza kuwa, asilimia kubwa ya walioshiriki katika zoezi hilo, wana uzito mkubwa kupita viwango vinavyokubalika kiafya. *(Makofi/Kicheko)*

Hali hii inatuweka katika mazingira ya kuweza kupata kwa urahisi magonjwa ya moyo na kisukari. Kufanya mazoezi ni utamaduni mzuri kwa ajili ya afya zetu. Kwa bahati nzuri, Bunge letu lina utaratibu wa kuwakutanisha Waheshimiwa Wabunge asubuhi, kwa ajili ya mazoezi. Wapo ambao ni wanachama hai wa Klabu ya Michezo ya

Bunge; wapo wanaopenda kutembea asubuhi au jioni au hata wanapotoka kwenye vikao vya Bunge. Hata hivyo, sio wengi wa kutosha tunaopenda kufanya hivyo. Hata kutembea hatupendi sana na tunatumia usafiri wa magari muda mrefu na hivyo kujinyima fursa ya mazoezi. Aidha, vyakula hivi tunavyokula hasa kwenye *Cafeteria* ni vya wanga na mafuta, hatupati au hatutaki kutumia matunda na mboga za majani kwa wingi. Napenda kuwapongeza kwa dhati, wale wote wanaojitahidi kufanya mazoezi au hata kutembea. *(Makofi)*

Napenda kutumia nafasi hii kumhimiza Mheshimiwa Spika, ile *gym* iliyopangwa kujengwa basi ijengwe mapema. Mwandishi mmoja Bwana Robin Sharma katika kitabu chake kinaitwa *Who Will Cry When You* Die! Anasema hivi:*"Those who don't make time for exercise must eventually make time for illness"*. Mazoezi ni muhimu kwa ajili ya kutunza afya zetu. Tujenge utamaduni wa kufanya mazoezi kwa ajili ya miili yetu. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumejiepusha na uwezekano wa kupata maradhi makubwa ya moyo na kisukari au hata yale magonjwa madogo madogo na ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, katika muda mfupi ujao, Waislamu nchini wataungana na Waislamu wenzao pote duniani katika mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Napenda kutumia fursa hii, kuwatakia Waheshimiwa Wabunge na Waislamu wote nchini, baraka za Mwenyezi Mungu na mfungo mwema. Aidha, kwa vile Sikukuu ya *Eid-el-Fitr* itafuata kabla ya kukutana tena, napenda vilevile kuwatakia Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla, *Eid-el-Fitr* iliyojaa neema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimezungumza vya kutosha, lazima sasa nihitimishe hotuba yangu na kuagana na Waheshimiwa Wabunge. Ninapenda nimalize kwa shukrani, za kwanza zikiwa kwako, Mheshimiwa Spika, umeliongoza Bunge hili kwa umahiri na ustadi wa hali ya juu sana. Nampongeza Naibu Spika na Wenyeviti, kwa uongozi imara, wa busara na wa haki, mliuonesha wa makini, umahiri na viwango vya hali ya juu, walivyojifunza kutoka kwako. Nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na watumishi wa Serikali, tuliokuwa nao hapa Dodoma, kwa kazi nzuri. Namshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka na watumishi wa Ofisi yake, kwa kutuhudumia vizuri sana. Nashukuru kwa kazi nzuri iliyofanywa na Waandishi wa Habari. Bila mchango wao, wananchi waliotutuma kuwawakilisha hapa Bungeni na waliotuweka madarakani, hawawezi kujua tunafanya nini kwa niaba yao. Nawashukuru Waandishi wa Habari wote kwa umoja wao, isipokuwa wale wa Gazeti la Uwazi kwa yale waliyoyafanya jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukrani za pekee ni kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi walivyoichangamsha Serikali. Wasipotuchangamsha tutalala na hatutaifikia kasi mpya, tuliyowaahidi wananchi, kwa hivyo, nawashukuru sana. Lakini nawaomba pia wasisahau mojawapo ya mafundisho yaliyo katika Hekaya za Esopo isemayo: "Ni rahisi kuwa shujaa ukiwa mbali." Mimi pia nimewahi kuwa Mbunge wa kawaida, bila kuwa Serikalini. Najua upo mvuto wa Mbunge, kutafuta ushujaa kwa kuishambulia Serikali, kwa kudhani yupo mbali na Serikali. Ukweli ni kuwa, katika nchi maskini kama yetu, si vyema Wabunge wakajihisi kuwa wako mbali na Serikali yao. Ukweli ni kuwa nchi hii

ni yetu sote na wa kuijenga ni sisi sote. Wa kuyabaini matatizo ya wananchi ni sisi sote na wa kuyatafutia ufumbuzi ni sisi sote. *(Makofi)*

Nimalizie, Mama mmoja alipenda sana kumtuliza mwanae mdogo kila akimpeleka kulala kitandani kwa kumwambia: “Lala mwanangu, ukihitaji chochote wewe niite tu. Nitamtuma Baba yako.” *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, wasirudi kwa wananchi na kauli kama hizo. Serikali inaendelea na mageuzi yake makubwa yanayopeleka madaraka makubwa kwa wananchi. Si madaraka ya maneno matupu, ni madaraka ya watumishi, madaraka ya fedha, madaraka ya vitendea kazi na madaraka ya kuamua. Lakini tukumbuke, pamoja na madaraka unakuja wajibu, nao ni wajibu wa kushughulikia matatizo mengi zaidi ya wananchi kwenye ngazi iliyo karibu nao. Kama vile Waheshimiwa Wabunge, walivyoichangamsha Serikali Kuu, nawaomba waende kuzichangamsha Halmashauri. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, waende kuwa chemchemi ya fikra mpya, wawe chachu ya maendeleo, washiriki ufumbuzi wa matatizo na kamwe wasiwe kama posta ya kuleta matatizo ya wananchi hapa Bungeni na kisha kurudisha majibu. Ni kweli hiyo ni mojawapo ya kazi za Mbunge, lakini isiwe ndiyo kazi pekee, tutachelewa. Narudia, wa kutambua shida za wananchi ni sisi sote na wa kuzishughulikia ni sisi sote kwa pamoja, kwa kushirikiana, twendeni tukawatumikie wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu, sasa liahirishwe hadi tarehe 31 Oktoba, 2006, Siku ya Jumanne, Saa 3:00 Asubuhi, litakapokutana hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Sina shaka mtakubaliana nami Waheshimiwa Wabunge kwamba, hiyo ni hoja kabambe ya kuahirisha Bunge. Kabla sijawahoji, kuna matangazo mafupi yafuatayo:-

Napenda tutambue kuwepo kwa familia ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mama Regina Lowassa, Bwana Fred Lowassa, Bwana Robert Lowassa na *Master*, kwa hiyo, huyu ndiyo mdogo mdogo tu Richard Lowassa. Wale ambao mmeshiriki vizuri kwenye Bunge na mnahudhuria mara kwa mara, mtakumbuka kwamba, Richard si mgeni sana, hapa kwa sababu mara kwa mara tunaonana naye pale nje, sielewi Mwenyezi Mungu, mambo haya sijui yanakuwaje? Hatujui hatma ya Richard, lakini Mungu aendelee kumsaidia inaelekea anapenda sana Bunge. Pia marafiki zao Bwana John Bakilana na Bwana Elias Lukumai. Karibuni sana na ahsante kwa

ushiriki wenu. Pia kwenye *Public Gallery* tunao wanachuo 41 wa Chuo cha Madini cha Mjini Dodoma. Naomba wasimame tafadhali, wale pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge, ambaye hakujitaja ananiomba nitangaze kwamba, kuna mgeni wake anaitwa Dr. Norman Sigalla, Mbunge wa Afrika Mashariki. Nadhani mnamfahamu huyo Mbunge. Karibu sana Dr. Norman. Aah namfahamu, lakini mimi nasoma hakuandika jina lake.

Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, ameniomba nimtambulishe mgeni wake, Bwana Muki Makame Ussi, Katibu Mwenezi wa Jimbo la Mtoni, karibu sana. Karibu yupo pale upande wa kushoto. Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude I. Mongella, anatangaza kwamba, kutakuwa na tamasha la Utamaduni la Wananchi waishio kwenye Visiwa vya Ukerewe, litakalofanyika Kijiji cha Makumbusho tarehe 19 nadhani mwezi wa Nane, 2006, kwa sababu ameandika wa saba itakuwa wa nane hadi tarehe 20. Naona ni *weekend* hii hii. Wabunge wote mnakaribishwa, hakuna kiingilio wala malipo, mtawaona wasanii 100 kutoka Visiwa hivyo pamoja na wale wana-mazingaombwe. Mheshimiwa Dr. Emmanuel J. Nchimbi, Naibu Waziri wa Habari na Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Harusi ya Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, anaomba kuwataarifu kwamba, kwanza anawashukuru kwa ushirikiano na anatangaza ratiba ifuatayo; ambayo Waheshimiwa Wabunge watakaoweza kushiriki, tafadhali waweze kushiriki.

Kwanza, *Send-off* itakuwa tarehe 9 Septemba, 2006 Malya Mwanza. Ndoa itafungwa tarehe 16 Septemba, 2006, ambayo Spika atahudhuria. Sherehe kwa Wana-Dar es Salaam itafanyika pale *NSSF Waterfront* tarehe 29 Septemba, 2006 kuanzia saa 12.00 jioni. Mtaona imepangwa ili isilete tabu au visingizio kwa wale ambao hawawezi kuhudhuria. Kwa hiyo, Dar es Salaam, jimboni Kahama huko na Malya Mwanza. Tunamtakia kheri, kwa niaba yenu namtakia kwa maandalizi ya siku muhimu sana. Waheshimiwa Wabunge, kikundi cha *Clouds Entertainment* kina muziki kabambe leo jioni kule *Kilimani Club*, watakuwapo akina Ray C, Banana Zolo, Mr. Nice, Mr. Ebbo, nadhani wamejaribu kutafuta wasanii wote walio nyota. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, ambao hamna haraka ya kuondoka jioni hii, sio ya utulivu sana inaweza ikachangamka. Mnakaribishwa sana na kiingilio ni bure kwa Waheshimiwa Wabunge wote. *Clouds* saa moja jioni pale Kilimani Klabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Adam K. A. Malima, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, wakutane Chumba Na. 231 ghorofa ya pili, mara baada ya kuahirishwa Mkutano huu.

Baada ya matangazo hayo, Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa muweze kuamua ile hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambayo ni ya kuliahirisha Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 05.38 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 31 Oktoba, 2006, Saa Tatu Asubuhi)*